

Vodacom Tanzania Public Limited Company

Taarifa ya mwaka

kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2022



Pamoja tunaweza



Maelezo ya Jumla

Taarifa ya Mwaka 2022 ya Vodacom Tanzania

Hii ni taarifa ya sita ya mwaka ya Vodacom Tanzania, na ya tano tangu kampuni iorodheshwe kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam tarehe 15 Agosti 2017.

Taarifa hii inatoa maelezo ya jumla ya biashara yetu, muundo wa biashara, mazingira ya uendeshaji, kupitia mikakati yetu, mafanikio ya mfumo wa undeshaji na utawala kwa mwaka wa fedha ulioanzia tarehe 1 Aprili 2021 hadi 31 Machi 2022. Utaratibu wetu wa kutoa taarifa ya mwaka umekuwa ukiongozwa na kanuni na masharti yaliyo katika Viwango vya Kimataifa vya Taarifa za Fedha (IFRS), Kanuni za Soko la Hisa la Dar es Salaam za mwaka 2016 na Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Mkaguzi huru, Ernst & Young ('EY') amekagua taarifa zetu za fedha za mwaka na kutoa hati safi. (ukurasa wa 88 hadi 90 kwenye nakala ya kiingereza).

Bodi imeshiriki kikamilifu katika uandaaji na uwasilishaji wa taarifa hii. Bodi inaanmini kuwa ripoti hii inaelezea masuala yote muhimu na inawasilisha maelezo yenye ulinganifu kuhusu utendaji wa kundi la Makampuni kwa kipindi husika na vilevile inatoa taswira halisi ya mikakati yetu ya utekelezaji.

Wakurugenzi wanaamini kuwa kuchapisha mipango mkakati ya Vodacom Tanzania, hakutaleta athari yeoyote ile katika medani za ushindani wa kibiashara. Bodi ilipitisha taarifa hii ya mwaka tarehe 12 Julai 2022.

Imesainiwa kwa niaba ya Bodi na:

Jiji (mstaafu) Thomas Mihayo
Mwenyekiti
12 Julai 2022

Hilda Bujiku
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji
12 Julai 2022

Azma yetu kuu ya kuongeza thamani katika jamii

Azma kuu ya Vodacom Tanzania ni 'kuunganisha jamii kwa kesho ilio bora'. Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu (UN SDGs) yanatoa taswira ya muonekano wa kesho ilio bora, kwa kuweka malengo ya muda mrefu ya kuondoa umaskini, kulinda mazingira na kuleta mafanikio kwa wote ifikapo mwaka 2030. Vodacom Tanzania ina nia ya kutimiza wajibu kama taasisi ya sekta binafsi katika kufikia malengo haya, kuunga mkono serikali, jamii, biashara na watu binafsi katika kujenga kesho iliyobora. Tunachangia kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa ya maendeleo kupitia biashara yetu kwa kuwezesha mawasiliano ya data, ujumbe, sauti na huduma za fedha na hivyo kutoa mchango muhimu katika kutimiza malengo ya maendeleo duniani.

Vodacom Tanzania imeainiwa na kuweka kipaumbele katika malengo nane ya maendeleo endelevu (yaliyorokewa mraba mweusi) ambayo tunaamini tunaweza kuwa na mchango chanya:



Yaliyomo

UTANGULIZI

- 02 Sisi ni nani
04 Thamani tulijojenga

BIASHARA YETU

- 06 Vodacom Tanzania kwa ufupi
07 Bidhaa na huduma zetu
08 Taarifa ya Mwenyekiti
10 Taarifa ya Kaimu Mkurugenzi Mtendaji

UTENDAJI WETU

- 14 Kutekeleza azma na wajibu wetu kwa jamii
18 Ufanisi wetu kifedha
24 Taarifa ya Wajibu wa Shirika kwa Jamii (CSR)

MFUMO WA KIUTAWALA

- 26 Viongozi wetu
28 Taarifa ya uongozi wa kampuni
30 Shughuli za uongozi wa kampuni
32 Taarifa ya Masuala ya Ujira

TAARIFA YA MKUTANO MKUU

- 34 Taarifa ya Mkutano Mkuu
39 Fomuya Mwatilishi

TAARIFA ZA ZIADA

- 41 Taarifa kuhusu umiliki
42 Taarifa za kampuni
Dai la Haki

Maelezo ya msingi

Tafadhalii zingatia kwamba , hii ni tafsiri ya taarifa ya mwaka kwa ufupi. Taarifa kamili ya mwaka imetolewa kwa lugha ya kiingereza. Iwapo kutatokea mkanganyiko wa tafsiri, taarifa ya kiingereza itatumika.

Asante kwa kutuamini



**Top Employer Africa &
Tanzania 2021**
Top Employer Awards 2021



Best Fintech App (M-PESA)
Tanzania Digital Awards 2021



Best Mobile Network
Tanzania ICT Awards 2021



**Most Reliable and Quality Network
Telecom Service Provider**
Consumers Choice Awards 2021



**Most Preferred Telecom Company
for Customer Service Experience in Tanzania**
Consumers Choice Awards 2021

Pamoja tunaweza

vodacom

Sisi ni nani

Vodacom Tanzania ni kampuni inayoongoza nchini Tanzania kwa kutoa huduma za mawasiliano kwa wateja wa matumizi binafsi na biashara ikiwa ni pamoja na huduma za simu sauti, data, ujumbe mfupi wa maneno na huduma za fedha kwa wateja zaidi ya milioni 15.4.

Vodacom Tanzania iliorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam mnano Agosti 15, 2017. Mmiliki mkubwa wa Vodacom Tanzania na kampuni zake tanzu (yaani 'Kundi la Kampuni za Vodacom') ni Vodacom Group Limited, kampuni iliyosajiliwa Afrika Kusini ambayo nayo inamilikiwa na Vodafone Group PLC ya Uingereza.



Azma yetu

Kwanini tupo

Kukuunganisha kwa kesho iliyo bora



Jamii ya Kidigitali
Kuwaunganisha watu na vitu kwenye intaneti



Kuwashirikisha watu wote
Kuhakikisha mawasiliano ya kidigitali yanapatikana kwa watu wote



Sayari yetu
Kupunguza athari kwa mazingira yetu

Dira yetu**Tunakoelekea na tunataka kuwa nani**

Kuwa kampuni ya kidigitali inayoongoza ambayo inawezesha jamii iliyounganishwa katika mtandao

Kuiunganisha jamii kwa kesho iliyobora

Kuwa mwajiri bora (mahali bora pa kufanyia kazi)

Kwa namna gani**Namna ya utekelezaji****01**

Kuaminiwa na wateja

03

Kufanya majaribio – kujifunza haraka

02

Kujenga mustakabali

04

Kutekeleza mambo yote kwa pamoja

**Mkakati wetu****Tunachotakiwa kufanya**

Kuthaminisha huduma ya data na fursa za kidigitali



Kuwa chapa inayoongoza. Kushikilia na kuongeza umiliki wa soko



Kuchochea ongezeko la wateja kupitia huduma ya M-Pesa



Kudhibiti gharama na kuwa na michakato yenye ufanisi



Kuendelea kuimarisha huduma kwa wateja wa matumizi ya biashara kupitia bidhaa zetu mbalimbali



Watu. Vipaji bora, kuzingatia taratibu bora

Thamani tuliyojenga

Ufanisi wetu

Wateja
milioni 15.4
↑ wameongezeka kwa 3.4%

Wateja katika soko¹
30.2%
nafasi ya kwanza

Wateja wa M-Pesa
milioni 6.8
↓ wamepungua kwa 7.6%

Mapato ya huduma
Shilingi bilioni 956.5
↓ yamepungua kwa 1.0%, ↑ ongezeko la 9.8%*

Mapato ya data
Shilingi bilioni 204.0
↑ ongezeko la 18.9%

Mapato ya M-Pesa
Shilingi bilioni 329.6
↓ yamepungua kwa 7.6%, ↑ ongezeko la 17.7%*

Faida ya uendeshaji
Shilingi bilioni 64.4
↑ ongezeko la 30.1%, ↑ ongezeko la 149.5%*

Gharama ya uwekezaji
Shilingi bilioni 173.9
↑ ongezeko la 42.1%

1. Ripoti ya robo mwaka ya mamlaka ya mawasiliano Tanzania (TCRA), ya mwezi Machi 2022.
* Takwimu zilizowekewa alama * kwenye ripoti hii zinawakilisha, makisio ya kiwango cha ukuaji au kupungua, iwapo tukiiondoa athari za tozo ya serikali kwenye miamala ya kutuma na kutoa fedha.

Kwa wateja wetu

Tumeweza mawasiliano kwa wateja
zaidi ya milioni **15.4**



Tumepanua wigo wa mtandao wetu wa teknolojia ya 3G na 4G kufikia 66.7% ya idadi ya watu (kwa kiwango cha 1Mbps)



Tumeweza mawasiliano jumuishi za kifedha kwa wateja wa M-Pesa zaidi ya milioni

6.8

Kampuni ya kwanza katika 'Net Promoter Score (NPS)' tukiwa tunaongoza

kwa alama 18

1. Kiwango cha kukua hakijaoneshwa kutokana na mabadiliko ya kanuni ya ukokotoaji.

Tumepanua mtandao wetu kwa kuongeza:

minara **143** – ya 4G
minara **43** – ya 3G
minara **32** – ya 2G



Kwa wanahisa wetu

Jumla shilingi

bilioni 549.3

zimelipwa kama gawio tangu Kampuni iorodheshwe kwenye soko la hisa miaka mitano iliyopita.



Kwa jamii yetu



Tumechangia jumla ya shilingi

bilioni 516.9

kwenye **fedha za umma kwa njia ya kodi na tozo**, masafa na tozo za mamlaka za udhibiti wa sekta

Zaidi ya shilingi

bilioni 1.0

zimetumika katika uwekezaji kwenye jamii, na kunufaisha zaidi ya watu milioni 1.5² nchini kote



Tumeunga mkono programu za Serikali kufikisha mawasiliano vijijini kwa kujenga

minara 283

katika kipindi cha miaka kumi iliyopita

Zaidi ya ajira

144 000³

zisizo za moja kwa moja zimetolewa kwa watanzania



Shilingi bilioni 395.3

zimetumika kwa ajili ya malipo ya bidhaa na huduma za wasambazaji wa ndani na makampuni **washirika takriban 500 nchini Tanzania**

Kuchoea kilimo cha kibashara – tumesajili zaidi ya wateja

140 000

katika mfumo wa M-Kulima

- Inajumuisha shughuli za kijamii zilizofanyika kupitia huduma zetu kwa jamii (CSR), na pia zilizogharimiwa na mfuko mama wa 'Vodafone Foundation', Uingereza, usajili namba 1193984.
- Inajumuisha pia huduma za kijamii zilizofanyika moja kwa moja kwa wateja wetu.
- Inajumuisha wafanyabiashara wadogo huria (Freelancers) na mawakala wa M-Pesa.

Kwa wafanyakazi wetu

Shilingi bilioni 63.8

zimetumika kwa wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo ya kuendeleza ujuzi




Tumetoa mafunzo ya kuijendezea kwa njia ya mtandao kwa zaidi ya wafanyakazi

500


Mafunzo yetu ya 'Doing What is Right' yenyе kozi tano, yalihudhuriwa na wafanyakazi **zaidi 484** yakilenga maadili na uzingatiaji wa utaratibu

Uwakilishi wa **40%** wa wanawake kwenye uongozi


Vodacom Tanzania kwa ufupi




Uwekezaji kwa miaka 4 (Shilingi billioni)




Wateja wa siku 90 (Millioni)




Idadi ya watu wanaofikiwa na mtandao wetu wa 3G na 4G




Idadi ya minara



Idadi ya minara ya 4G



Idadi ya watu wanaofikiwa na mtandao wetu wa 4G



Bidhaa na huduma zetu

Tuna wateja zaidi ya **milioni 15.4**
wanaotumia bidhaa na huduma zetu



Huduma kwa matumizi ya
wateja binafsi na kidigitali



M-Pesa



Matumizi ya wateja wa
Biashara



Sauti

- Simu za kiganjani

Data

- Modemu za broadband
- Intaneti kwa simu

Ujumbe mfupi

- Ujumbe mfupi wa maneno na programu za mitandao ya kijamii

Huduma za ziada

- Burudani na michezo (muziki, video na bahati nasibu)
- Elimu (habari, vipindi vya dini na matangazo ya kidigitali)
- Huduma binafsi (My Vodacom app, tovuti yetu na Njipige tafu)
- Afya (Elimika, afya call)
- Huduma za usafiri (Paisha)

Huduma kwa wateja

- Kituo cha mawasiliano
- Dawati la huduma kwa wateja
- Maduka ya Vodacom
- Huduma binafsi (My Vodacom app, USSD code, M-Pesa app)
- Huduma za kidigitali (kupitia mitandao ya kijamii, tovuti, Whatsapp na Live Chat app)
- Viashiria kwa wateja (ujumbe ibukizi)



Kuweka na kutoa fedha

Kwa mawakala zaidi ya 120 000

Kuhamisha na kupokea fedha kati ya wateja wetu

Kutuma pesa ndani ya nchi na kimataifa (IMT)

Mifumo ya malipo ya kielektroniki

- Kadi za kielektroniki 'M-Pesa Visacard'
- Mfumo wa malipo wa 'Lipa kwa Simu'
- Mteja kwenda kwenye Biashara 'C2B'
- Biashara kwenda kwa Mteja 'B2C'
- Biashara kwenda kwa Biashara 'B2B'

Huduma za kifedha

- Huduma ya mikopo ya Songsisha
- Akiba na mikopo (M-Pawa, Halal Pesa)¹
- Akaunti za akiba za vikundi (M-Koba)
- Mikopo ya muda ya mawakala
- Huduma za bima

1. Akaunti za akiba za Halal Pesa zinafuata miongozo ya Sharia.



Simu za kiganjani

- Sauti
- Intaneti
- Ujumbe mfupi wa maneno
- Video

Uunganishaji

- Pasi waya
- Kwa waya
- VPN
- Mkongo, intaneti maalumu na ya kushirikiana

Kusimamia shughuli kwa mtandao

- Intaneti ya Vitu ('IoT')
- APN kwa ajili ya makampuni

Usalama, 'cloud' na kuunganisha ('hosting')

Bidhaa na huduma maalum

- Huduma kwa wakulima 'Connected Farmer' au 'M-Kulima'
- Huduma kwa mashule 'VodaShule', 'Connected education'



Taarifa ya Mwenyekiti

Jaji (mstaafu) Thomas Mihayo

Ni furaha kwangu kuwasilisha ripoti ya tano ya pamoja ya Vodacom Tanzania tangu kuorodheshwa kwa Kampuni katika Soko la Hisa la Dar es Salaam mnano Agosti 2017. Mpaka sasa, Vodacom ni kampuni pekee ya mawasiliano ya simu iliyoordheshwa katika Soko la Hisa nchini Tanzania, na ninaamini ni moja ya kampuni chache katika soko hilo inayozingatia misingi ya utoaji wa ripoti ya pamoja.

Tulipokuwa tukiendelea kuimarika kutoka kwenye athari za kiuchumi na kijamii za janga la UVIKO-19, kama nilivyoziainisha kwenye taarifa yangu ya mwaka uliopita, ilibidi pia tushughulikie changamoto za kibiashara zilizosababishwa na tozo mpya katika miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu za kiganjani, zilizoanza katikati ya mwezi Julai 2021. Pia, mazingira ya biashara yaliendelea kuwa na ushindani mkubwa. Kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza, ninaamini Kampuni imetuwa na matokeo ya kuridhisha. Mafanikio haya yameakisi uimara wa mfumo wetu wa biashara, uthabiti wa timu yetu ya menejimenti na ubora wa utekelezaji wa mipango yetu katika kukuza huduma zetu jumuishi za kidigitali na kifedha.

Nia ya kutekeleza azma yetu ya 'kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora', ni kichocheo cha utendaji thabiti wa kampuni yetu. Kampuni imeendelea kuchochaea mabadiliko ya kijamii na kiuchumi na kuhakikisha uimara na ukuaji endelevu, kwa kuwekeza katika miundombinu ya mtandao, kuanzisha bidhaa na huduma za kibunifu na za gharama nafuu, kuwahudumia wateja wenye mahitaji ya kifedha ya muda mfupi, kuongeza upatikanaji wa vifaa janja kwa bei nafuu na kuendelea kutoa huduma bora kwa wateja. Pamoja na ushindani katika soko,

Vodacom imeendelea kuongoza kwa kuwa na wateja wengi zaidi katika soko na katika kipimo cha kuridhika kwa wateja, 'Net Promoter Score', huu ni ushahidi wa uthabiti wa utekelezaji na ubora wa makkati wake.

Katika taarifa ya Mwenyekiti ya mwaka uliopita, niligusia umuhimu wa kuendeleza mahusiano chanya kati ya Kampuni na serikali, ili kufikia matokeo mazuri kwa njia ya majadiliano. Limekuwa ni jambo la kutia moyo mwaka huu, kuona maendeleo makubwa katika majadiliano kati ya Kampuni na taasisi mbalimbali za serikali, na bunge – kuititia kamati zake, kuhusu masuala yanayohusu sekta ya mawasiliano, na mtazamo wa kampuni kuhusu masuala hayo. Tumefanya majadiliano yenye tija na wizara yenye dhamana ya mawasiliano, pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuhusu huduma ya mawasiliano ya simu. Sambamba na hili, tumepiga hatua nzuri katika kutatta masuala yanayohusu kodi kuititia majadiliano na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Kuanzishwa kwa tozo katika miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu za kiganjani mwaka huu, kuliathiri jitihada za kuendeleza huduma jumuishi za kifedha nchini Tanzania. Tozo hizi ziliongeza kwa kiasi kikubwa gharama kwa wateja kufanya miamala ya fedha kwa njia ya simu za kiganjani, na kusababisha

wateja zaidi ya milioni 1.3 kuacha kabisa kutumia huduma zetu za M-Pesa. Mbali na kuathiri ukuaji huduma jumuishi za kifedha, tozo hizo ziliathiri mapato ya Kampuni kwa makadirio ya kiasi cha shilingi bilioni 103.8. Katika taarifa hii, tumetoka maelezo ya ziada kuonesha makisio ya ufanisi wa utendaji wa biashara katika mwaka, pasipo athari za tozo. Badiliko hili ni muhimu ili kuongeza uwazi na kuonesha uhalisia wa matokeo ya uendeshaji wa kampuni. Licha ya athari za kibiashara za tozo nilizoainisha hapo juu, nimefurahishwa na utayari wa serikali kujadiliana kuhusu suala hili, ambapo mwezi Septemba 2021, tozo zilipunguzwa kwa 30%, na tena zikapunguzwa zaidi kwa 43% kuanzia 1 Julai 2022, kufanya jumla ya punguzo la 60% tangu tozo hizo kuanzishwa. Tuna imani kuwa, kwa kushirikiana na serikali, tutapata suluhisho litakalochagiza upatikanaji zaidi wa manufaa yatokanayo na teknojologia, na huduma jumuishi za kifedha.

Katika kutekeleza azma yetu, tumetekeliza programu kadhaa. Kati ya hizo, ninajivunia programu iliyoitukuka ya M-Mama. Programu hii inakusudia kupunguza vifo yya kina mama na watoto, kwa kutoa huduma ya usafiri kwa wanawake wajawazito kwenda katika vituo yva afya, katika maeneo ya vijijini hapa Tanzania. Tunaendesha mradi huu kwa kushirikiana na

Serikali ya Tanzania na 'Vodafone Foundation'¹. Programu yetu ya majaribio, tuliyoifanya katika Kanda ya Ziwa ilikuwa ya mafanikio, ambapo tulihudumia walengwa 12 000 ikiwa ni pamoja na wanawake na watoto wachanga. Pia jamii ilinufaika kutokana na mafunzo yaliyotolewa kwa wafanyakazi wa sekta ya afya na madereva waliohusika katika programu hii. Kwa niaba ya Bodii na wafanyakazi wote wa Vodacom, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ambaye mapema mwezi Aprili 2022, alitenga muda wake adhimu kuzindua awamu ya pilii ya programu hii. Nimefurahishwa na hatua iliyofikiwa, ambapo programu hii sasa itajumuisha mikoa 14, yenye takribani nusu ya idadi ya watanzania. Hatua hii ni uthibitisho wa azma yetu ya dhati, kutekeleza wajibu wetu kwa jamii kwa ushirikiano na washirika wetu.

Vodacom Tanzania, ikiwa ni sehemu ya kundi la makampuni ya 'Vodacom Group' iliyoasiliwa nchini Afrika Kusini, ni mwajiri anayetoa fursa sawa kwa wote, kuwawezesha wafanyakazi kutimiza ndoto zao. Ni kwa msimamo huu, Bodii iliamua pia ripoti za mwaka za Kampuni, zizumuise takwimu za uwiano wa kijinsia za wafanyakazi. Katika kutekeleza lengo hili, mwaka huu tuliwakaribisha wajumbe wawili wapya katika timu ya viongozi waendeshaji wa Kampuni.

Mwezi Novemba 2021, tulinmeua Bi Hilda Bujiku kuwa Mkurugenzi mpya wa fedha, kuanzia tarehe 1 Januari 2022; akichukua nafasi ya Bw Jacques Marais ambaye baada ya kutumikia Kampuni kwa miaka mitano akiwa Mkurugenzi wetu wa fedha, amehamia katika kampuni nyiningine tanzu ndani ya kundi la makampuni la Vodacom. Ninaona fahari kubwa kwa uteuzi wa Hilda, ambaye mbali na kuwa mtanzania wa kwanza, pia ni mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo. Kabla ya kushika nafasi hii, Hilda alikuwa Mkurugenzi msaidizi wa fedha. Uteuzi wake unaakisii mpango wetu madhubuti wa kuandaa viongozi.

Kufuatia kujuzulu kwa Hisham Hindi, ambaye baada ya miaka mitano ya utumishi mzuri katika Kampuni, alihamia kampuni dada ya Vodafone Hispania, Sitholizwe (Sitho) Mdlalose aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu. Kabla ya uteuzi huo, Sitho alikuwa Mkurugenzi wa Fedha wa Vodacom Afrika Kusini. Sitho ameleta uzoefu na maarifa makubwa yaliyoleta ufanisi katika nafasi hii muhimu. Mwezi Julai 2022, Sitho amerudi Afrika Kusini kuongoza Kampuni dada ilio kubwa zaidi ya Vodacom South Africa. Mriithi wake atatangazwa wakati upasao. Katika kipindi cha mpito, Hilda Bujiku – Mkurugenzi wa Fedha, ameteuliwa na Bodii kukaimu nafasi ya Mkurugenzi mtendaji. Kwa niaba ya Bodii,

ninatambua kipaji na uzoefu ambaa Sitho ameleta katika Kampuni. Katika muda mfupi ambaa ameiongoza kampuni, amebuni mikakati imara ambayo sote tunaamini itasaidia kuimarisha utendaji, na nafasi yetu ya kwanza katika soko, katika muda wa katii na muda mrefu. Namna ya uongozi ya Sitho imekuwa rasilimali muhimu, katika kuimarisha uhusiano na waduu wanaozunguka biashara yetu, ikiwa ni pamoja na watunga sera, wateja na wafanyakazi.

Kwa niaba ya Bodii, ninatoa shukrani zetu za dhati kwa Sitholizwe na Jacques kwa mchangano wao mkubwa katika Kampuni hii, na tunawataki mema katika shughuli zao mpya. Wote wanathibitisha fursa ya kukua 'GROW' na Vodacom, ambazo zinatufanya tuwe mionganoni mwa waajiri bora nchini.

Tunatiwi moyo na muelekeo chanya wa siku za usoni kutokana na kuimarika kwa uchumi wa Tanzania, kunakochewa na udhibiti imara wa mfumuko wa bei na kuimarika kwa sekta ya utalii, ambayo kama nilivyogusia kwenye taarifa ya mwaka uliopia, iliathiriwa sana na kuenea kwa UVIKO-19. Ingawa viashiria hivi vinatupa matumaini, bado kuna mashaka juu ya athari za kiuchumi kutokana na mgogoro kati ya Urosi na Ukraine, ambao tarayi umeathiri vibaya bei za vyakula na nishati duniani. Licha ya kuwepo mashaka haya, bado ninaamini kuwa Vodacom

viongozi watendaji katika kutimiza kwa usahihi wajibu wao wa kazi, maadili na wajibu kwa jamii. Ninajivunia kuwa tuna Bodii inayojumuisha wakurugenzi watendaji, wakurugenzi wasio watendaji na wakurugenzi huru, wenye maarifa, uzoefu, mitazamo mbalimbali na jumuishi kijinsia. Kwa kuzingatia hayo yote, ninapenda kuwashukuru wajumbe wenzangu wa Bodii kwa mchangano wao muhimu kwa Kampuni, na pia kuwashukuru viongozi watendaji na wafanyakazi wote wa Kampuni kwa kuendelea kujituma katika kuwezesha matokeo yanayoridhisha hasa, tukizingatia changamoto za mazingira ya kibiaresha yaliyopo.

Ninawasihi na kuwahimiza, waduu wetu wote, kutenga muda na kusoma ripoti yetu ya mwaka ya fedha ulioishia Machi 2022, ili kuelewa matokeo ya utendaji wa biashara na namna yaliyofikiwa, na inapowezekana, tafadhalii tupatii mrejesho.

Jaji (mstaafu) Thomas Mihayo
Mwenyekiti

12 Julai 2022

“

Pamoja na ushindani katika soko, Vodacom imeendelea kuongoza kwa kuwa na wateja wengi zaidi katika soko na katika kipimo cha kuridhika kwa wateja cha, 'Net Promoter Score', huu ni ushahidi wa uthabiti wa utekelezaji na ubora wa mkakati wake.”

Tanzania ina mikakati sahihi, uongozi thabiti na mifumo imara, kuhakikisha ukuaji endelevu na uimara wa Kampuni.

Mwaka huu, Bodii iliendelea kutimiza majukumu yake kadiri ya muongozo wa uendeshaji wa Bodii uliowekwa. Nilitimiza wajibu wangu wa kuhakikisha kuwa Bodii inafanya usimamizi makini na huru, wa utendaji na mwelekeo wa kimkakati wa Kampuni, pamoja na kusimamia

1. Kwenye ripoti hii ya mwaka, 'Vodafone Foundation', ina maanisha mfuko wa jamii wa Kampuni mama ya 'Vodafone Group', mfuko uliosajiliwa nchini Uingereza kwa namba 1193984.



Taarifa ya Kaimu Mkurugenzi Mtendaji

Hilda Bujiku

Mapema mwezi Aprili, tulitanua wigo wa programu yetu ya M-mama, inayotoa huduma ya usafiri kwenda kwenye vituo vya afya kwa kina mama wajawazito maeneo ya vijiji. Huduma hii sasa itapatikana kwenye mikoa yenye takribani nusu ya idadi ya watanzania wote. Programu hii inayoendeshwa kwa ushirikiano na serikali, ina lengo la kupunguza vifo vya mama na mtoto. Ikiendelea mafanikio ya programu hiyo yaliyofikiwa kanda ya ziwa – Mwanza na Shinyanga.

Katika mwaka wa fedha 2022, tuliongeza kasi ya utekelezaji wa mkakati wetu mahususi – unaokusudia kufanikisha malengo ya kibashara na pia kuisaidia jamii. Tulitekeleza mipango mbalimbali, ikiwa ni muendelezo wa mikakati ya kuisaidia serikali, jamii na biashara, iliyoanzishwa wakati wa kilele cha mapambano dhidi ya UVIKO-19. Mipango iliyotekelzeza ilikuusudia kutimiza wajibu wetu kwa jamii, na kuilindu hadhi yetu ya 'kampuni inayoheshimika'. Ninaridhishwa na matokeo ya utekelezaji wa programu yetu ya kuunganisha huduma ya mawasiliano vijiji, ambapo tayari kuna minara 1 680¹, ikijumuisha minara 283 iliyojengwa kwa ushirikiano na serikali kuitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (Universal Communications Service Access Fund). Programu hii ni muhimu katika kupunguza mgawanyiko wa kidigitali kwa kuwezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa gharama nafuu. Mawasiliano yanasaidia katika utekelezaji wa programu zetu za kutimiza wajibu wetu kwa jamii zinazolenga elimu, afya, mazingira na kilimo.

Mbali na biashara yetu kuu ya huduma ya mawasiliano, tuliendelea kuihudumia jamii tukitumia uwezo na mifumo yetu ya kidigitali. Huduma yetu ya M-Kulima iliwezesha malipo yasiyo fedha taslimu kwa zaidi ya wakulima 140 000 waliosajiliwa, ikiwanufaisha kwa kasi ya malipo na usalama kwa pande zote husisa katika miamala. Huduma yetu ya M-Mama imewasaidia

wanawake wajawazito na watoto, zaidi ya 12 000 katika maeneo ya Kanda ya Ziwa – Mwanza na Shinyanga tangu kuanzishwa kwake mnamo mwaka 2013. Mnamo Aprili, tumezindua rasmi programu hii nchini kote, na sasa itapatikana katika mikoa 14.


Tukiangalia utendaji wetu wa kifedha, mapato yetu ya huduma yaliathiriwa na tozo mpya zilizowekwa katika huduma za fedha kwa simu kuanzia Julai 2021. Ijapokuwa mapato ya huduma yaliongezekwa kwa 12% katika robo ya kwanza ya mwaka kabla ya tozo kuanzishwa, mapato ya huduma ya mwaka mzima yалиshuka kwa 1.0%. Pasipo athari za tozo zinazokadirwa kufikia shilingi bilioni 103.8, mapato ya huduma yaliongezekwa kwa 9.8%. Ongezeko hilo lilichagizwa na ufanisi mkubwa katika huduma za data, sambamba na ongezeko la huduma za kidigitali, kufuatia uwekezaji wetu katika mtandao wa data. Licha ya shinikizo katika mapato ya huduma, faida ya uendeshaji iliongezekwa kwa 30.1% (149.5%*) ikifananishwa na mwaka uliopita, kufikia kiasi cha shilingi bilioni 64.4, ikichochewa na hatua zilizochukuliwa za kupunguza gharama za uendeshaji. Tunatiwa moyo kwa uamuzi wa serikali kupunguza tozo kwa 30% mwezi Septemba 2021, na punguzo la 43% kuanzia Julai 1, 2022. Punguzo hili linafanya jumla ya punguzo kufikia 60% toka kuanzishwa kwa tozo hizi. Hatua hii inategemewa kupunguza gharama kwa wateja wetu. Tutaendelea kushirikiana na kutoa maoni kwa serikali kuhusu

mwenendo wa tozo. Tunaamini kwamba, kuitia fursa za ukuaji katika M-Pesa, tunaweza kukuza huduma jumuishi za kifedha.

Utekelezaji wa malengo yetu kimkakati
Huu ni mwaka mwingine ambapo Vodacom Tanzania iliendelea na utekelezaji thabiti wa mikakati yake. Tulipiga hatua madhubuti katika utekelezaji wa mipango yetu ya kimkakati, huku tukipambana na changamoto zilizojitekeza, ikiwemo athari za tozo katika miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu za kiganjani. Tukiongozwa na lengo letu la kufanya biashara huku tukisaidia jamii, mkakati wetu tunaouita 'System of Advantage', unaotumia vyema uwezo wetu kiteknolojia, uliendelea kuwezesha huduma mbalimbali na zenyetofauti kwa wateja wetu.

Kuthaminisha huduma za data na fursa za kidigitali
Tumeendelea kuzalisha matokeo mazuri katika kuthaminisha huduma ya data, na kuongeza msukumo wa matumizi ya data na huduma za kidigitali. Utekelezaji wetu ulijikita katika uwekezaji katika mtandao – hususan mtandao wa 4G, kuongeza usambazaji wa simu janja na kuendelea kutoa ofa mbalimbali kwa wateja wetu, kuwezesha huduma, kuwaridhisha wateja na hatimaye kuongeza mauzo. Matokeo chanya katika nyanya ya data, ni muhimu katika kusukuma ajenda yetu ya ukuaji na ujumuishi kidigitali.

1. Kadiri ya vigezo na utaratibu wa ndani wa Kampuni.



“

Huu ni mwaka mwingine ambapo Vodacom Tanzania iliendelea na utekelezaji thabiti wa mikakati yake. Tulipiga hatua madhubuti katika utekelezaji wa mipango yetu ya kimkakati, huku tukipambana na changamoto zilizojitokeza, ikiwemo athari za tozo katika miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu za kiganjani.”

Licha ya changamoto zilizoathiri utendaji wetu kifedha, tunamatumaini na fursa zilizopo katika soko na hivyo tumeendelea kuwekeza katika mtandao. Mwaka huu, tulivekeza jumla ya shilingi bilioni 173.9, ni ongezeko la 42.1%, kuboresha mtandao wetu. Uwekezaji huu ulielekezwa katika kuongeza minara ya 4G, uboreshaji wa mtandao uliopo, na kuimarishe miundombinu yetu ya TEHAMA. Tuliongeza minara mipya 143 ya 4G na kuboresha zaidi ya minara 530 ya zamani, tukiongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za 4G kufikia 50% ya watu, ikilinganishwa na 42% tulioifikia mpaka mwaka jana. Nimefurahishwa na hatua ya serikali ya kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT), katika simu janja, ambayo sambamba na uwekezaji wetu endelevu katika mtandao, pamoja na mbinu zetu za kibunifu za kuongeza upatikanaji wa simu janja, viliongeza upatikanaji wa vifaa janja kwa bei naafuu. Uwekezaji huu ulichangia ongezeko madhubuti la 18.9% katika mapato ya data za simu, wakati

mapato ya huduma za kidigitali na huduma za ziada yaliongezekwa kwa 46.6% hadi shilingi bilioni 36.3. Ongezeko la mapato, lilitokana na kuongezekwa matumizi, huduma zilizoboreshwana ongezeko la watumiaji. Zaidi ya hayo, watumiaji wa simu janja waliongezekwa kwa 12.1% hadi kufikia milioni 4.1, ambaao ni sawa na 54.2% ya wateja wa data, ongezeko la pointi za asilimia 13.5 ikilinganishwa na uwiano wa mwaka uliopia. Ongezeko la watumiaji wa simu janja, lilichangia ukujai wa matumizi ya data kwa mteja kwa 22.3%, kufikia wastani wa gigabaiti 1.7 kwa mwezi. Uwekezaji katika mtandao na simu janja, ulichagiza ongezeko la 20.8% katika matumizi ya jumla ya data, wakati matumizi ya data kwa mtandao wa 4G yaliongezekwa kwa 59.0%, yaki akisi uhitaji mkubwa na fursa katika huduma za data na kidigitali katika soko.

Tulifunga mwaka tukiwa na wateja wa data milioni 7.6, sawa na 49.5% ya wateja wetu. Idadi hii ya wateja ni pungufo kwa 1.2% ikilinganishwa na

Shilingi bilioni 64.4

Faida ya uendeshaji
ongezeko la 30.1% (149.5%*)

Shilingi bilioni 173.9

Gharama ya uwekezaji
ongezeko la 42.1%

mwaka uliopia. Upungufo huu ulichangiwa na kufungiwa huduma kwa zaidi ya wateja 200 000 ambaao hawakuwa wamekamilisha usajili kwa alama za vidole kulingana na matakwa ya kanuni za usajili wa wateja.

Kuungeza kasi ya ongezeko la wateja kupitia M-Pesa

Kupitia uhusiano wetu na kundi la Makampuni la Vodacom na 'M-Pesa Africa', tumeendelea kupanua wigo wa huduma zetu na kunufaika na usoefu wa kampuni hizi, ambaao umechangia M-Pesa kuendelea kuongoza kwa kuwa na 39.6%¹ ya idadi ya wateja katika soko. Ubora wa bidhaa zetu na utekelezaji thabiti wa mikakati ya kibaashara umetusaidia kupata wateja wapya ambaao wamechangia kuziba pengo la wateja milioni 1.3 walioacha kutumia huduma za M-Pesa kufuatia kuanzishwa kwa tozo ya miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu za kiganjani. Kwa kuongzeza, huduma za kifedha, huduma ya malipo kwa simu na, huduma ya

1. Ripoti ya robo mwaka ya mamlaka ya mawasiliano Tanzania (TCRA), ya mwezi Machi 2022.

Taarifa ya Kaimu Mkurugenzi Mtendaji inaendelea

kutuma na kupokea fedha kimataifa (IMT) zimeendelea kuzoleka na kuwa huduma za msingi kupitia M-Pesa. Na muhimu zaidi, hazikuathiriwa kwa kiasi kikubwa na athari za tozo za miamala.

Tunaamini kwamba, uwepo wa huduma bunifu na nafuu, ni kichocheo cha huduma jumuishi za kifedha. Bidhaa yetu ya mkopo ya Songesha imendelea kufanya vizuri kwa kuwezesha wateja kukamilisha miamala, kukiwa na ongezeko la 10.9% ya mikopo iliyotolewa, na pia ongezeko la 6.8% la wateja wa Songesha. Thamani ya mikopo iliyotolewa kwa mawakala iliongezeka kwa zaidi ya 120%, ikiwa na wastani wa shilingi 230 000 kwa kila mnufaika kwa mwazi. Pia tulijikita katika kurahisisha huduma ya malipo kwa wateja wetu, kupitia mfumo wa 'Lipa kwa simu', tukiwa na wafanyakishara zaidi ya 40 000 wanaopokea malipo kwa mfumo huo. Katika kipindi cha mwaka huu, miamala yenye thamani ya zaidi ya shilingi triliioni 1.7 ilifanyika, ambayo ni ongezeko la zaidi ya 25% ikilunganishwa na mwaka uliopenda. Pia, huduma yetu ya kutuma na kupokea fedha kimataifa iliendelea kutoa mchango mkubwa katika ujumuishi kifedha, na kuongeza fedha

katika mfumo wetu wa M-Pesa. Miamala ya kimataifa yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 850 ilifanyika, ikiwa ni ongezeko la zaidi ya 40% kwa mwaka.

Iapokuwa tulipiga hatua ya kuridhisha katika kufanya majaribio, kuzindua na kuongeza bidhaa na huduma mbalimbali mpya katika mfumo wa M-Pesa, biashara yetu ililathiriwa na kuanzishwa kwa tozo katika miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu za kiganjani. Tulifanikiwa kuongeza idadi ya wateja wetu wa M-Pesa kufikia milioni 7.8 mwishoni mwa robo ya kwanza ya mwaka, hata hivyo, idadi hii ilipungua na kufikia wateja milioni 6.5 mwishoni mwa robo ya pili ya mwaka, ikiwa ni athari ya utekelezaji wa tozo. Uendeshaji wetu thabiti wa biashara pamoja na punguzo la awali la tozo kwa 30% mnamo Septemba 2021, vilichangia kuongezeka kwa idadi ya wateja wetu hadi kufikia milioni 6.8 mwishoni mwa mwaka wa fedha.

Kwa upande mwingine, mapato ya M-Pesa yalipungua kwa 7.6% hadi shilingi bilioni 329.6. Ukiondoza athari za tozo, ongezeko la mapato ya M-Pesa lilifikia 17.7%*, likichagizwa na kuponuka kwa wigo wa huduma ya M-Pesa. Mwaka huu, jumla ya miamala yenye thamani ya zaidi ya shilingi triliioni 60 ilichakatwa katika mfumo wa M-Pesa, ikiakisi umuhimu wa huduma yetu katika mfumo wa kifedha nchini.

Kuendelea kuimarishe huduma kwa wateja wa kibashara

Mapato katika huduma zetu kwa wateja wa kibashara, yameendelea kuwa na ongezeko thabitibidi hususanii katika huduma ya data za simu za kiganjani na uunganishwaji kwa njia ya waya. Tumekuwa na maendeleo mazuri katika biashara ya uunganishwaji kwa njia ya waya, kukiwa na ongezeko la wastani la 20% la minara mipyili ya iliyounganishwa, na wastani wa wateja wapya 100 kila mwazi. Mapato ya huduma ya kuunganishwa kwa njia ya waya yameendelea kuongezeka, na bado kuna nafasi ya kukua zaidi kutokana na fursa zilizopo katika soko. Pia, mapato ya biashara yetu ya mfumo wa IoT (vitu vilivyounganishwa kwa Intaneti) yaliongezeka kwa zaidi ya 25% kwa mwaka. Na huduma hii ina fursa kubwa ya kukua zaidi sambamba na kutimiza azma yetu ya kuingiza Tanzania katika ulimwengu wa kidigitali. Tumeendelea kupiga hatua zaidi katika kusambaza huduma zetu za kilimo na elimu kidigitali, kwa ushirikiano na kampuni mshirika ya Mezzanine. Mwishoni mwa mwaka, tulikuwa na wakulima wadogowadogo zaidi ya 140 000 waliosajiliwa katika mfumo wetu wa M-Kulima, kukiwa na vyama vya ushirika (AMCOS) takribani 300. Mafanikio katika huduma ya M-Kulima ni kipaumbele kwetu, kwa kuwa inahudumia sekta muhimu kiuchumi na pia, inatupa fursa ya kuboresha maisha ya familia nyingi.

Chapa inayoongoza. Kulinda na kuongeza umiliki wa soko

Japokuwa kuna ushindani mkali kibashara, tumeendelea kuwa na alama nzuri katika vipimo mbalimbali vya viashiria vya kuridhika kwa wateja, ikiwa ni ishara ya uimara wa chapa yetu.

Baadhi ya viashiria hiyivo ni:

● Idadi ya Wateja katika Soko:

Tumeendelea kuongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wateja katika soko kwa 30.2%¹ na M-Pesa kwa 39.6%¹ ya wateja wa huduma ya fedha kwa simu.

● Net Promoter Score (NPS):

Tumeendelea kuongoza katika kipimo cha kuridhika kwa wateja, 'NPS', tukiwa na pointi 18 zaidi ya mtoa huduma anayefuatia. Pia, tunaongoza kwenye 'NPS' ya ubora wa mtandao kwa pengo la pointi 14 na 'NPS' ya huduma kwa wateja kwa pengo la pointi 15.

● TUZO:

Tumepokea tuzo kadhaa kwa kutambua ubora wa huduma zetu. Baadhi ya tuzo hizo ni **Consumer Choice Awards 2021** ya 'Kampuni ya mtandao wa simu yenye mtandao bora na wa kuaminika zaidi', na ya 'Kampuni ya mawasiliano ya simu inayopendwa zaidi kwa huduma bora kwa wateja nchini Tanzania'. **Tanzania Digital Awards 2021** kwa 'Kampuni ya mawasiliano ya simu ya mwaka', 'Aplikesheni bora ya huduma za fedha kwa simu' (aplikesheni ya M-Pesa), 'Kampuni ya mawasiliano ya simu yenye ubunifu zaidi ya mwaka' na 'Kampuni ya mawasiliano ya simu yenye huduma bora kwa wateja', **Tanzania ICT Awards 2021** ya 'Mtandao bora wa simu', zikishamirishwa na **tuzo za kitaaluma** za 'Taarifa bora zaidi ya fedha zilizowasilishwa kwa mwaka 2021' – katika kundi la biashara na usambazaji, iliyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA) na cheti cha 'Mwajiri bora Tanzania 2022' na cheti cha 'Mwajiri bora Afrika 2022', vinavyotolewa na kampuni ya kimataifa ya masuala ya uajiri ya 'Top Employers Institute'.

Udhibiti wa gharama na ufanisi

Kwa miaka kadhaa, tumetekeleza mikakati madhubuti katika kupunguza ongezeko la gharama za uendeshaji biashara ili kuwezesha ufanisi wa kampuni kifedha. Ufanisi huu unawezeshwa na mikakati ya kudhibiti ukujai wa gharama na pia, kutumia uzoefu na faida za uhusiano na makundi ya Kampuni washirika za Vodacom na Vodafone. Mwaka huu, mikakati hiyo ilipunguza gharama za uendeshaji za zaidi ya shilingi bilioni 40, na kufanya jumla ya fedha



1. Ripoti ya robo mwaka ya mamlaka ya mawasiliano Tanzania (TCRA), ya mwezi Machi 2022.

zilizookolewa kuwa shilingi bilioni 167.8 katika miaka mitano iliyopita. Uokoaji huu wa gharama ulichangia ufanisi katika matokeo ya utendaji wa Kampuni, licha ya ongezeko la gharama katika baadhi ya maeneo kutokana na ushindani wa kibashara na changamoto za usafirishaji na usambazaji duniani.

Watu: Vipaji bora, utekelezaji bora

Ili kutekeleza malengo yetu ya kimkakati tunahitaji kuwa na vipaji na ujuzi sahihi, na utamaduni sahihi, mazingira bunifu na huduma bora kwa wateja. Tumeendeleza mwelekeo wetu thabiti katika kuimarisha utamaduni wetu wa kuwashirikisha wafanyakazi kwa lengo la kuwawezesha kujisimamia mtu mmoja mmoja na ki-idara. Ni jambo linalotia moyo kuona kwamba Vodacom Tanzania PLC imepata alama za juu kabisa katika kundi la makampuni ya Vodafone katika kipengele cha umoja na ushirikishwai katika kazi. Na, kwa mwaka wa tano mfululizo, Vodacom Tanzania ilipewa cheti kama Mwajiri bora Tanzania 2022 na Mwajiri Bora Afrika 2022.

Azma yetu ya kuwawezesha wazawa na kuajiri watu wa makundi mbalimbali, ilipiga hatua zaidi mwaka huu kuelekea katika malengo yetu ya 2023 kuhusu uwakilishi wa kijinsia na jumuishi: mwishoni mwa mwaka 40% ya menejimenti ilikuwa ni wanawake, na pia aliteuliwa Mtanzania na mwanamke wa kwanza kuwa Mkurugenzi wa Fedha. Viongozi wote waandamizi isipokuwa wawili ni Watanzania, hivyo kuwa na wastani wa 84.6% ya uwakilishi wa viongozi waandamizi, kutoka 30.8% miaka mitano iliyopita.

Vilevile, tumesherehekeea mwaka wa kumi bila vifo vya ajali kazini. Hatua hii inaonesha mafanikio yetu katika kuweka mazingira salama kazini kwa wafanyakazi na watoa huduma wetu.

Mtazamo wetu kimkakati

Ninajivunia sana mafanikio tuliyofikia, na mipango tunayoendelea nayo ya kukuza biahsara ili kuzalisha faida, kulinda mtaji wa wanahisa, na ustawi wa wafanyakazi, huku tukitoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania na kuboresha viwango vya maisha ya jamii.

Tunatazamia kuendeleza azma yetu ya kuwaunganisha Watanzania ili wawe na maisha bora siku zijazo. Lengo letu limeegemeeria katika mihimili mitatu ambayo ni jamii iliyounganishwa kidijitali, huduma jumuishi kwa wote, na kulinda sayari kwa kupunguza athari za mazingira. Tunaamini kuwa ongezeko la kasi ya matumizi ya data, kuenea kwa simu janja, huduma za kidijitali na za kifedha, ni muhimu katika kutekeleza lengo tulilokusudia. Na, kwa kutekeleza wajibu wetu kwa jamii, tutaleta chachu ya ukuaji wa uchumi, na hivyo kuongeza fursa zaidi ya ukuaji wa biahsara.

Tunatekeleza mkakati wetu kuititia mbinu madhubuti chini ya mfumo wetu uitwao 'System of Advantage'. Mfumo huu unatuwezesha kuwapatia wateja wetu huduma mbalimbali na zenyet utofauti, zikiwezesha na uwezo wa hali ya juu wa mifumo yetu. Mfumo wetu wa 'System of Advantage' unatuwezesha utoaji wa huduma za kidigitali na kifedha zinazozingatia mahitaji ya mteja mmojammoja, na hivyo katuwezesha kutoa huduma bora kabisa kwa wateja. Mkkatii huu ni muhimu katuwezesha kukabiliana na ushindani na kuvumbua fursa mpya za ukuaji.

Tutaweka msisitizo maalum katika kuitumia vyema **thamani na nafasi ya chapa yetu katika soko**, – nia yetu ikiwa ni kuhakikisha kuwa chapa yetu inaendelea kuwa chapa inayopenda na yenye kuaminiwa na wateja wetu, na pia wadau wote. Tutaendeleza kuhakikisha wateja wetu wanapata huduma zenyet ubora wa hali ya juu, na pia kutimiza matarajio ya wadau wetu wote, huku tukitekeleza wajibu wetu kwa jamii. Tunatamani chapa ya Vodacom iwe chapa pendwa iliyo, ndani ya miyo ya kila mdau.

Tutalinda kwa bidii nafasi yetu ya uongozi katika huduma za mawasiliano ya simu – tukizingatia mtazamo wa wateja wetu kuhusu thamani ya bidhaa zetu, kuchocheara matumizi na kuthaminisha huduma za data, kupanua wigo wa huduma za kidigitali ili kuwapatia wateja sababu za kutumia huduma ya data, kupanua mtandoa na kusambaza vifaa janja, kuongeza ofa binafsi, hususan, ofa za data. Umuhimu wa mkakati wetu jumuishi wa kidigitali, unachagizwa na mahitaji makubwa ya huduma za data na za kidigitali sokoni. Bado tuna fursa ya kuongeza usambazaji wa simu janja kwani huduma hiyo kwa sasa inatumiwa na 53.9% tu, ya watumiaji wetu wa data. Tutaendelea kuwekeza katika mifumo mikubwa ya data, yenye kuwezesha utoaji wa ofa bora za data kwa wateja wetu, ili kuendeleza uongozi wetu wa umiliki wa soko, matumizi zaidi ya data na kuhakikisha mahusiano endelevu ya huduma na wateja wetu. Tutaendelea kujizatiti kulinda nafasi yetu sokoni, pamoja na kuwa washirika muhimu kwa wateja wetu bila kuathiri uthamani wa soko.

Ni matamano na lengo letu **kuongeza wigo na kuikuza huduma ya M-Pesa** – kwa kuendeleza mafanikio tuliyoyapata katika huduma zetu za kiasili na za kisasa tulizonazo, huku tukichocheara uanzishwaji wa huduma na bidhaa mpya za kibunifu, na pia tukiongeza idadi ya watumiaji wa M-Pesa. Kupitia uhusiano wetu na Kampuni yetu mama, 'Vodacom Group' tutaendelea kunufaika na kutumia utaalamu kutoka kwa, kuihuisha aplikesheni yetu ya M-Pesa kuwa ya ubora wa juu, ikichochewa na uwezo mkubwa tulionao kiteknolojia. Aplikesheni hii ya kisasa,

itaendelea kutoa huduma mbalimbali za mikopo na akiba, malipo na huduma ya kutuma na kupokea fedha, burudani, kurahisisha manunuzi binafsi na hivyo kuchocheara huduma jumuishi za kifedha. Ni dhamira yetu kuendelea kuchangia kukuza ujumuishi kifedha nchini.

Katika eneo la wateja wa Kibashara, tutashughulikia fursa zilizopo katika biahsara ya uanganishwaji kwa waya kwa kujitofautisha na watoa huduma wengine, ili kuwapatia wateja wetu huduma bora na salama za data majumbani na ofisini. Pia, tutaendeleza **ubunifu na kuongoza katika eneo hili la wateja wa kibashara**, kwa kulenga mahitaji yanayotokana na changamoto za kisasa za kiteknolojia katika biahsara, na vilevile kutoa huduma zinazozingatia mahitaji maalum ya kisekta kupitia mfumo wa IoT. Pia, tunakusudia kuongeza ufanisi katika matumizi ya rasilimali zetu, ikiwemo kuingia **mikataba ya biahsara ya kukodisha sehemu ya rasilimali zetu**, ambazo zinatumika kwa sehemu tu ya uwezo wake.

Tutaendeleza juhudii za kuhakikisha ustahimilivu wa gharama za uendeshaji na kuchukua hatua madhubuti kuongeza mapato, ili kuwezesha **kampuni kuzalisha faida** na kuongeza ufanisi wa matumizi ya mtaji. Sambamba na hili, tutaendeleza jadi yetu kwa kuhakikisha tunawaendeleza wafanyakazi, **tunakuwa na timu ya watu wanaofanya kazi kwa ufanisi**.

Wakati tunaendelea na utekelezaji wa mkakati wetu, tunatambua changamoto zinazoweza kuleta na milipuko ya UVIKO-19, pamoja na athari za vita ya Ursusi na Ukraine. Hata hivyo, tunakusudia na tunatumaini tutakuza biahsara yetu katika muda wa kati, huku tukiendelea kuiunganisha Tanzania kwa kesho iliyo bora.

Shukrani

Katika kuhitimisha, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Bodii kwa kuni amini na kuni pa jukumu la kuongoza kampuni katika kipindi cha mpito. Na pia, timu ya viongozi waandamizi, wafanyakazi wote na washirika wetu wa biahsara, kwa kunikaribisha na kuni ahidi ushirikiano wa dhati, katika jukumu nililokabidhiwa. Sina shaka kuwa Vodacom Tanzania imejiweka mahali pazuri kimkakati na nina amini kuwa, timu hii imejipanga vizuri kutekeleza wajibu wake kwa jamii – kuiongoza Tanzania katika ulimwengu wa kidigitali na kubadili maisha ya watanzania kupitia teknolojia.

Pamoja Tunaweza.

Hilda Bujiku
Kaimu Mkurugenzi Mkuu

12 Julai 2022

Kutekeleza azma na wajibu wetu kwa jamii

Azma ya Vodacom Tanzania ni 'kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora'. Tunapambana kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuunganisha watu na vitu kwenye intaneti, kusukuma mbele jitihada za maisha jumuishi kwa wote na kupunguza athari za mazingira.

Tunaamini kuwa kuboresha huduma za mawasiliano ya sauti na data, na kuimarishe upatikanaji wa huduma za kidigitali kwa wote, ni zana muhimu katika kuchochoea mageuzi ya kiuchumi na kijamii na hivyo kutoa mchango mzuri kuelekea kufikiwa malengo ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa.




Tukiwa sehemu ya kampuni ya Vodafone na Kundu la makampuni la Vodacom, tumedhamiria kujikita katika maeneo matatu yanayolenga kuchangia katika kufikiwa kwa malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu (UN SDG):

Kuchoea **maisha jumuishi kwa watu wote**




Kuunda **Jamii ya kidigitali**



Kulinda **Sayari yetu kwa kupunguza athari za mazingira**

Kupitia shughuli zetu katika maeneo haya matatu, tumeweka kipaumbele kutoa mchango chanya katika Malengo nane, yaliyowekwa kivuli.





Jamii Iliyounganishwa Kidigitali

Ni muhimu kuongeza matumizi ya TEHAMA hapa Tanzania, ili kuleta mageuzi kutoka uchumi wa kilimo asilia kwenda uchumi wa kipato cha katika unaendeshwa kwa uimara wa ujuzi na maendeleo ya viwanda vya katika. Sekta ya mawasiliano ya simu za kiganjani imechangia katika malengo ya maendeleo ya taifa kwa kuwezesha upatikanaji wa huduma jumuishi za kidigitali. Na pia sekta hii, bado ina nafasi ya kuchangia zaidi kwa kuongeza upatikanaji wa huduma muhimu, kuongeza uzalishaji katika sekta mbalimbali za kibashara, na kufungua fursa jumuishi za kiuchumi. Tunaendelea kupunguza ombwe la kidigitali kwa kuongeza upatikanaji wa huduma za kidigitali kupitia uwekezaji wetu katika kupanua miundombinu ya mawasiliano hasa katika maeneo ya vijijiini, kuwezesha upatikanaji wa simu janja za bei nafuu, kuwezesha upatikanaji wa vifurushi vya gharama nafuu na vilevile upatikanaji wa mifumo ya kidigitali inayotatua changamoto za kijamii, kiuchumi na kimazingira.

Kutoa huduma za mtando wote

- ✓ Mwaka huu, tumewekeza shilingi bilioni 173.9 katika upanuzi wa wigo na kuongeza ubora wa mtando wetu. Tumeongeza minara mipyä 20 vijijiini na kuboresha zaidi ya minara 185 na kufanya kuwa ya teknolojia ya 3G na 4G. Miongoni mwa minara mipyä ya vijijiini, minara 14 imejengwa kwa ubia na serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, 'Universal Communication Services Access Fund – UCSAF'. Mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka, tulikuwa na jumla ya minara 1 680 vijijiini¹, ikiwa ni pamoja na minara 283² iliyojengwa kwa ushirikiano na UCSAF katika kipindi cha miaka kumi iliyopita ya ushirikiano wetu. Hadi kufikia mwisho wa mwaka, 66.7%³ ya idadi ya watu wamefikiwa na mtando wote teknolojia ya 3G na 4G, ikiwa ni matokeo ya uwekezaji wetu endelevu katika upanuzi na uboreshaji wa mtando wetu.
- ✓ Tumeendelea kuchochaea usambazaji wa simu janja ili kuwawezesha watu wengi zaidi kupata huduma za data na kidigitali. Hadi kufikia mwisho wa mwaka, watumiaji wa simu janja walifika milioni 4.2, ikiwa ni ongezeko la 12.1% kwa mwaka. Ongezeko la watumiaji wa simu janja miongoni mwa watumiaji wa data lilifika 54.2%, ikiwa ni ongezeko la alama za asilimia 13.5 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Licha ya changamoto za usafirishaji na usambazaji duniani, zilizosababishwa na janga la UVIKO-19, tulifanikia kupiga hatua nzuri katika kuchochaea usambazaji wa simu janja, ikichagizia na uamuza wa serikali kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye simu janja. Tunaendelea kushirikiana na serikali na wabia wetu katika kutambua fursa za kusisimua mahitaji na kuwezesha upatikanaji wa simu janja kwa bei nafuu.
- ✓ Tumeendelea kuhamasisha ujumuishaji katika huduma za kidigitali kwa kutumia vifurushi yetu vya gharama nafuu vinavyotolewa chini ya ofa za mwavuli wa 'Kwa Ajili Yako' zinazowezeshwa na mifumo yetu ya 'CVM' na 'machine learning'. Mwaka huu, zaidi ya wateja milioni 7 wametumia ofa za 'Kwa Ajili Yako Tu' zinazotolewa ki-kanda kila mwezi, idadi hii ya wateja inaakisi mafanikio ya mkakati huo.
- ✓ Pia tumeendelea kuwezesha upatikanaji wa huduma kupitia huduma ya mikopo wa 'Nipige Tafu'. Huduma hii inawawezesha wateja kupata huduma za simu ikijumuisha data, kwa kukopa muda wa maongezi au bando, na kurejesha pindi wanapopata uwezo wa kuongeza muda wa hewani. Kwa mwaka huu, zaidi ya wateja milioni 8.8 walinufaika na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 68.6, ongezeko la 58.3% ikilinganishwa na mikopo iliyotolewa mwaka uliopita.

Huduma za Kidigitali

- ✓ Jukwaa letu la kilimo la M-Kulima linaloendeshwa kwa ushirikiano na kampuni ya Mezzanine, sasa limesajili wanachama ambao ni wakulima wadogo zaidi ya 140 000 na kuwaunganisha na huduma mbalimbali katika mnyororo wa thamani, unaowezesha upatikanaji wa taarifa, huduma na masoko kupitia SMS na 'App', na pia kuwezesha malipo kwa ucharaka na usalama. Wakulima walio katika orodha hivi sasa, wapo katika mikoa 15 hapa nchini Tanzania na wanajishughulisha na mazao ya pamba, mahindi, maharage, alizeti, tumbaku, dengu, kahawa, choroko, zabibu na bidhaa za maziwa. Tunaendelea na juhudi za kuongeza idadi ya wakulima waliosajiliwa katika makundi ya mazao yote yaliyopitishwa na serikali.
- ✓ Huduma za kuunganisha vitu na intaneti 'IoT' inajumuisha mifumo mbalimbali, ambayo inachochaea ufanisi na kurahisisha matumizi. Tunazo huduma mbalimbali, ikiwa ni pamoja na, mita janja za umeme na maji – ambazo zinapunguza au kuondoa kabisa hitaji la msoma mita kuingiza kwa mikono rekodi za matumizi, na hivyo kuongeza usahihi wa bili, na kuleta ufanisi katika ukusanyaji wa mapato; na vilevile mifumo ya usimamizi wa mali ambayo inaboresha matumizi ya rasilimali na kutoa taarifa mbalimbali za uendeshaji wa kifaa husika ikiwa ni pamoja na uhitaji wa kufanya matengenezo na pia kuimarisha usalama kwa kubainisha mahali kifaa au mali ilipo.

1. Tafsiri ya minara iliyopo 'vijijiini' ni kadiri ya taratibu za ndani za Vodacom kuhusu mipaka na si lazima kwa maana ya eneo la kijiografia. Pia idadi ya minara iliyokwisha ripotiwa, inaweza kubadilika kutohakana mapitio na uainishaji mpya.
 2. Tafsiri ya 'kijijiini' ni kwa kadiri ya taratibu za ndani za mipaka za Vodacom. Ileweke kwamba minara iliyojengwa kwa ubia na UCSAF si yote iko 'maeneo ya vijijiini' kijiografia, bali imejengwa sehemu ambazo zinauhitaji na hazingweza kupata huduma hiyo kwa kusubiri maamuzi ya kibashara.
 3. Kipimo kwa Mbps 1
 4. Hapo awali litambulika kama Benki Ya Posta Tanzania

Huduma jumuishi za kifedha

- ✓ Tumeendelea kupiga hatua katika kukuza huduma jumuishi za kifedha kupitia bidhaa zetu bunifu za M-Pesa. M-Pesa imeendelea kuwa huduma ya kifedha inayowafikia wateja wengi zaidi nchini Tanzania, ikiwa na wastani wa wateja milioni 6.8 kila mwezi, waliochakata miamala zaidi ya bilioni moja, yenye thamani ya shilingi trillioni 61.8 kwa mwaka. Licha ya athari zilizotokana na kuanzishwa kwa tozo katika miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu za kiganjani, tuliendelea na tunadhamiria kuendelea kuunga mnkon, ajenda ya kukuza huduma jumuishi za kifedha nchini. M-Pesa inatoa huduma mbalimbali za kifedha kwa wateja wanaotumia na wasiotumia huduma za kibenki, ikiwesha urasimishaji wa miamala ya kifedha, hasa kwa jamii isiyotumia huduma za kibenki.
- Kupitia pochi ya huduma za M-Pesa, M-Pawa na Halal Pesa tunawapatia wateja wetu huduma ya 'akaunti ya akiba mkononi'. Mwaka huu, amana zenye thamani ya takribani shilingi bilioni 170 ziliwekwa kwenye akaunti za M-Pawa na Halal Pesa.
- Bidhaa yetu ya akiba ya M-Koba, inayoendeshwa kwa ubia na 'Tanzania Commercial Bank'⁴ (TCB), imeandaliwa kimsingi kwa ajili ya kuhudumia vyama vya akiba na mikopo katika jamii. Mwaka huu, akiba zenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 50 ziliwekwa katika akaunti za M-Koba.
- Tumewawezesha wateja wa M-Pesa kupata mikopo ya M-Pawa na Songesha, ambayo ina wateja zaidi ya milioni 3.8 walipopata mikopo.
- Tumeongeza wigo wa huduma zetu za kifedha kwa kutoa mikopo kwa mawakala wetu, ambapo zaidi ya mawakala 70 000 walinufaika na mikopo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 210.7 ya Songesha na ya muda maalum, iliyotolewa kuwezesha biashara zao, ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma kwa wateja wetu.

Kutekeleza azma na wajibu wetu kwa jamii inaendelea



Huduma jumuishi kwa wote

Tunafanya kazi ya kupambana na umaskini na kuongeza usawa nchini Tanzania kuititia jitihada mbalimbali, ikijumuisha programu zetu za kutoa elimu na huduma ya afya kwa usawa, na kuunga mkono biashara mpya za kibunifu za ki-teknolojia. Mchango wa jitihada zetu katika maeneo haya ni ziada ya manufaa muhimu yaliyopatikana kuititia shughuli zetu za kuhamasisha huduma jumuishi za kifedha na kilimo zilizopo chini ya mipango ya Jumuiya ya Kidigitali.



Upatikanaji wa huduma ya elimu kwa wote

- ✓ Kwa kutoa huduma bora na inayoaminika ya mtandao wa data nchini, tunawawezesha wateja ya Vodacom kuvifika vyanzo bora vya taarifa na mafunzo ya kielimu kuititia intaneti. Katika mwaka huu, programu yetu ya Uwajibikaji kwa Jamii, iliwekeza shilingi milioni 758.8 ili kuwezesha upatikanaji wa zana za kujifunzia, bure kuititia Mfumo wetu wa 'Instant School', uliohudumia wanufaika zaidi ya 185 000.

Upatikanaji wa huduma za afya kwa wote

- ✓ Tumefurahishwa na hatua tuliyopiga katika programu yetu ya M-Mama ambayo imewasaidia wanawake wajawazito na watoto wachanga zaidi ya 12 000 katika maeneo ya kanda ya Ziwa ya Mwanza na Shinyanga tangu kuanzishwa kwake mnamo mwaka 2013. Programu hii inaendeshwa kwa ushirikiano na serikali katika juhudi za kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa kutoa huduma ya usafiri wa kwenda vituo vya afya katika maeneo ya vijijini. Mnamo Aprili, tuliongeza wigo wa programu hii kufikia mikoa 14, inayojumuisha nusu ya idadi ya watu nchini.
- ✓ Katika kuunga mkono jitihada za kupunguza vifo vya watoto na kustahimili majanga, vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 58.5 vilitolewa kwa hospitali ya Mkomaindo Masasi, mkoani Mtwara. Msada huu ni wa vifaa tiba vya huduma kwa watoto wachanga wenye kuhitaji uangalizi maalum na mama wajawazito. Hospitali hii inahudumia takribani watoto wachanga 100 wanaozaliwa kabla ya wakati.

 Taarifa zaidi kuhusu programu za afya na elimu zimeripotiwa katika ripoti ya CSR katika **ukurasa 24 wa 25**

Kusaidia biashara zinazochipukia za kiteknolojia

- ✓ Kuititia programu yetu ya 'Digital Accelerator' iliyoindiliwa mwaka 2020 kwa kushirikiana na Smart Lab, mdau mweneupye uzoefu katika teknolojia zinazochipukia, tumeendelea kusaidia na kutoa ushauri kwa makampuni 15 yaliyoteuliwa katika nyanja za teknolojia ya fedha, elimu, afya, mazingira na biashara ya mtandao. Lengo ni kuwasaidia vijana wa Kitanzania kubadili maono yao kuwa biashara zenye thamani ambazo zitatao nafasi za ajira na kutatua changamoto za kijamii. Mafanikio ya duru ya kwanza ya jitihada hizi yanmetutia moyo kuzindua duru ya pili mwaka huu.

Kuunga Mkono Mafunzo ya Teknolojia kwa Wasichana

- ✓ Mwaka huu, tumeendelea na programu yetu ya '#codeLikeAGirl' inayowalenga wasichana wenye umri kati ya miaka 14 – 18, ikiwa na kusudio la kuwajenga na kuwaongezea wasichana uujuzi wa kiteknolojia katika kutengeneza programu za kidigitali zitakazochangia maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi. Hatua hii inalenga kuhamasisha wasichana kuchukua masomo ya TEHAMA na 'STEM' ambapo washiriki katika programu hii wanabainishwa kuititia shule za sekondari nchini. Mwaka huu, jumla ya wasichana 306 walihuduria mafunzo hayo ya wiki moja, na kupata maarifa ya awali ya lugha za kompyuta na kuandaa programu ikiwa ni pamoja na 'HTML' na 'CSS', lugha ya kompyuta kwa ajili kuandaa kurasa za tovuti. Tangu kuanzishwa kwake, zaidi ya wasichana 1 000 wamehuduria programu hii, ambao wanakua sehemu ya ipaji vyetu katika nyanja ya teknolojia.



Sayari

Tumeendelea kupunguza athari za mazingira zinazotokana na shughuli zetu za kibashara kwa kuwekeza katika masuala ya tabianchi ikiwamo mitandao na mifumo inayotumia nishati kidogo, kupunguza taka katika mnyororo wetu wa thamani, kuongeza unyumbuwa wa tabianchi kwa kutunza misitu na kuhakikisha kuwa tunafuata kikamilifu masharti yote ya utunzaji wa mazingira.

Mabadiliko ya tabianchi, na ufanisi katika matumizi ya nishati na maji

- ✓ Tumeendelea kuchoecha jithhada za kuongeza ufanisi katika matumizi ya nishati na maji, na kupunguza hewa ya ukaa kwa kuboresha vituo vyetu vya data. Maboresho hayo yametokana na mradi uliotekelawa kubadili jenereta za zamanii, na matumizi ya mifumo ya kisasa ya 'cloud' yenye ufanisi zaidi. Mwaka huu, matumizi ya nishati yalipungua kwa 3.3% hadi 16.4GWh, matumizi ya mafuta yaliongezekwa kwa 5.8% hadi lita milioni 1.7, na matumizi ya maji yaliongezekwa kwa 6.4% hadi kilolita 26.9. Matumizi ya nishati yamepungua kutokana na ufanisi katika shughuli za mtandao, wakati ongezeko la matumizi ya mafuta linachochewa na matumizi ya jenereta kutegemeana na upatikanaji wa umeme wa gridi. Kwa upande mwiningine, matumizi ya maji yameongezeka kutokana na wafanyakazi wengi kurudi kufanya kazi ofisini kwa kuwa athari za UVIKO-19 zimepungua ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Kupunguza uzalishaji taka

- ✓ Utaratibu wetu wa muda mrefu wa kuwahimiza wateja kutumia njia za kielektroniki kuongeza muda wa maongezi, kama vile M-Pesa, mashine za kutolea pesa (ATM) na Vodafasta na kubadili utaratibu wa kutumia vocha za karatasi zimechangia kuepuka

matumizi ya wastani wa tani 134 za karatasi mwaka huu, na kufikia wastani wa tani 736 za karatasi katika miaka mitano iliyopita.

- ✓ Vilevile, matumizi ya laini ndogo za simu zilizotengenezwa kwa malighafi inayooza kirahisi, kumeepusha matumizi ya plastiki na taka za plastiki kwa wastani wa tani 15 mwaka huu, na kufikia wastani wa jumla ya tani 122 za taka za plastiki katika miaka mitano iliyopita.

Utunzaji wa bioanuwai na tabianchi

- ✓ Mwaka huu, tulitumia shilingi milioni 104.5, kuendezea mradi wetu wa Kijanisha Dodoma, kwa lengo la kuongeza uelewa na kuhamasisha jamii kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi na bioanuwai na vilevile kutunza miti tuliyopanda mwaka uliopita. Jamii zimenufaika si kutokana na miti tuliyopanda tu, bali pia kuptia programu za kujenga uwezo kwa zaidi ya wanajamii 800, kutoka katika vikundi nya vijana na wanawake wajasiriamali kuhusu matumizi ya teknolojia endelevu za nishati kwa ajili ya shughuli za uzalishaji wa uchumi. Hivi sasa, mradi huu una miti zaidi ya 96 000 katika jiji la Dodoma.

Viashiria vya uendelevu wa biasara	Kipimo	Machi 22	Machi 21	Machi 20	Machi 19	Machi 18
Idadi ya wafanyakazi	Idadi	560	569	551	548	537
Idadi ya wafanyakazi wanawake	Idadi	209	203	204	200	212
Wanawake kwenye Kamati ya Uongozi (EXCO)	%	38.5	36.4	30.8	36.4	30.8
Wanawake kwenye menejimenti (wakuu wa vitengo na EXCO)	%	40.0	41.2	41.2	41.2	42.9
Wafanyakazi wanawake	%	37.3	35.7	37.0	36.5	39.5
Jumla ya gharama zilizotumika kugharimia wafanyakazi	(Shi bn)	63.8	61.6	57.7	59.4	55.3
Jumla ya matumizi katika mafunzo	(Shi bn)	0.2	0.7	1.0	0.7	0.8
Vifo wakati wa kazi	Idadi	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna
Net Promoter Score'	Nafasi	Kwanza	Kwanza	Kwanza	Kwanza	Kwanza
Kiwango cha kuridhika cha ushikishwaji wafanyakazi ('engagement index')	%	85	86	86	85	85
Wateja wote (siku 90)	Idadi ('000)	15 368	14 861	15 513	14 133	12 899
Wateja wa M-Pesa (kwa mwezi)	Idadi ('000)	6 833	7 395	6 685	6 989	6 369
Wateja wa data (kwa mwezi)	Idadi ('000)	7 603	7 695	7 687	7 892	7 345
Gharama ya uwekezaji	(Shi bn)	173.9	122.4	154.6	171.4	159.7
Jumla ya Kodi na makato yaliyolipa serikalini	(Shi bn)	516.9	429.7	434.8	391.5	379.1
Jumla ya mikopo ya muda wa hewani kwa wateja	(Shi bn)	68.6	43.3	38.2	34.6	53.1
Jumla ya thamani ya miamala iliyopita kwenye M-Pesa	(Shi bn)	61.9	69.2	58.9	50.0	43.1
Wanufaika wa mikopo ya songesha	Idadi ('000)	3 776	3 541	2 001		
Minara vijijiini (UCSAF)	Idadi	283	260	217	199	188
Wateja wetu walio kujifunza	%	57	56	53	53	47
Matumizi ya karatasi yaliyoepukwa kwa kutumia vocha za kielektroniki	Tani	134	140	175	155	132
Matumizi ya plastiki yaliyoepukwa kwa kutumia 'laini - SIMcard' ndogo	Tani	15	22	30	31	25

Ufanisi wetu kifedha

Taarifa za Jumla	2022	2022 Ukiondoa athari za tozo*	2021	% ya mabadiliko mwaka hadi mwaka	% Mabadiliko Mwaka hadi Mwaka ukiondoa athari za tozo*
					2022
Mapato ya huduma (Sh milioni)	956 515	1 060 359	966 014	(1.0)	9.8
Ambapo					
Mapato ya huduma za simu kwa sauti ¹	286 985		302 037	(5.0)	
Mapato ya M-Pesa	329 557		356 801	(7.6)	
Mapato ya data za simu ²	203 985		171 585	18.9	
Mapato ya Kidigitali & Huduma za ziada ³	36 294		24 749	46.6	
Mapato ya simu zinazoingia	48 105		58 141	(17.3)	
Mapato ya ujumbe mfupi	28 861		31 877	(9.5)	
Jumla ya mapato	971 025	1 074 870	974 391	(0.3)	10.3
Mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu (EBITDA) (Sh milioni)	300 341	359 432	316 134	(5.0)	13.7
Kiwango cha EBITDA (%)	30.9	33.4	32.4	(1.5)pp	+1.0pp
Mapato kabla ya riba na kodi (Sh milioni)	64 434	123 525	52 095	30.1	149.5
Gharama za uwekezaji ⁴	173 955	173 955	122 447	42.1	42.1
Asilimia ya gharama za uwekezaji (%)	17.9	16.2	12.6	+5.3pp	+3.6pp
Nafasi yetu kwa idadi ya wateja wa soko ⁵ (%)					
Idadi ya wateja hai/amilifu ⁶ (maelfu)	15 368		14 861	3.4	
Idadi ya wateja hai/amilifu wa M-Pesa kwa siku 30 ⁷ (maelfu)	6 833		7 395	(7.6)	
Wateja hai/amilifu wa data ⁸ (maelfu)	7 603		7 695	(1.2)	
Dakika zilizotumika kwa mwezi ⁹	232		194	19.6	
Wastani wa kipato kutoka kwa mteja - ARPU ¹⁰ (shilingi kwa mwezi)	5 132	5 705	5 259	(2.4)	8.5
Idadi ya wafanyakazi	560		569	(1.6)	
Idadi ya minara					
4G	1 963		1 820	7.9	
3G	2 868		2 825	1.5	
2G	3 388		3 356	1.0	
Ulinganishi wa NPS ¹¹ (nafasi kulingana na washindani)		Kwanza		Kwanza	

* Katika ripoti hii, namba na alama za asilimia zilizowekewa alama **, zinaashiria ongezeko iwapo tukiondoa athari za tozo ya serikali katika miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu ya kiganjani.

Maelezo:

1. Mwaka uliopita, 'Mapato ya huduma ya simu kwa sauti' yaliyoripotiwa yalijumuisha mapato ya Huduma ya Mkopo wa muda wa hewani 'Nipige Tafu' (2021: shilingi bilioni 9.5) ambapo sasa yameripotiwa chini ya mapato ya 'Kidigitali na Huduma za Ziada'. Hakukuwa na athari katika jumla ya mapato kutokana na uainishaji huu mpya.
2. Mwaka uliopita, 'Mapato ya Data za Simu' yaliyoripotiwa yalijumuisha matumizi na mapato kutokana na Huduma za Ziada (VAS) (2021: shilingi bilioni 15.3) ambayo yameripotiwa tofauti kuanzia mwaka wa fedha wa 2022 Hakukuwa na athari katika jumla ya mapato kutokana na uainishaji huu mpya.
3. Inajumuisha mapato ya 'Huduma ya Mkopo wa muda wa hewan' - Nipige Tafu, ambayo hapo awali yaliripotiwa chini ya 'Mapato ya huduma za simu kwa sauti', na 'Huduma za Ziada' - VAS yalijokuwa yakiripotiwa chini ya 'Mapato ya data ya simu'. Huduma hizo mbili kwa sasa zimeweka pamoja na zinariipotiwa kama 'Mapato ya Kidigitali na Huduma za Ziada'. Hakukuwa na athari katika jumla ya mapato kutokana na uainishaji huu mpya.
4. Matumizi ya gharama za uwekezaji kama asilimia ya mapato.
5. Kwa mujibu wa takwimu za mawasiliano za robo mwaka ya Mamlaka ya Udhibili wa Mawasiliano Tanzania za Machi 2022.
6. Wateja wanautumia huduma wanatokana na jumla ya idadi ya watumiaji simu walioitunga huduma yoyote katika miezi mitatu iliyoipita. Hii ni pamoja na wateja wanaolipa ada ya kila mwezi ambayo inawapa hakiki ya kutumia huduma husika hata kama kiuhalisia hawaitumii huduma hiyo na wale wateja ambao wanawasiliana nje ya mtando.
7. Wateja hai wa M-Pesa wanatokana na idadi ya watumiaji wa kipekee walioitunga M-Pesa na kufanya miamala inayotozwa katika kipindi cha mwezi.
8. Wateja hai wa data wanatokana na idadi ya watumiaji wa kipekee wanaoalisha data inayotolewa bili katika mwezi. Pia ni pamoja na watumiaji katika mpango wa pamoja wa watumiaji au ambao wanautumia APN ya shirika na watumiaji ambao warmetengewa bando ya data inayozalisha mapato katika mwezi. Mtumiaji anachukuliwa kuwa hai kama analipa ada ya mwezi kulingana na mkataba kwa huduma hii au ametumia huduma hii katika mwezi huo.
9. Dakika za matumizi kwa mwezi hukokotolewa kwa kugawanya jumla ya dakika zilizotumika kwa mwezi kwa wastani wa watumiaji wa dakika hizo katika kipindi hicho.
10. ARPU inakokotolewa kwa kugawa wastani wa mapato ya huduma kwa mwezi kwa wastani wa jumla ya wateja kwa mwezi katika kipindi hicho.
11. Net promoter score ('NPS') ni kipimo kuanza – 100 hadi 100 ambacho kinaonesha utayari wa wateja kupendekeza bidhaa au huduma za mtoe huduma kwa watu wengine. Inatumiika kama kigezo cha kupima hali ya kuridhika kwa wateja na bidhaa au huduma za mtoe huduma imani ya wateja kwa chapa hiyo. Kwa kila mtoe huduma, majibu yanakusanywa kutoka kwa wateja ambao wanautumia bidhaa au huduma zake kama njia kuu au mbadala ya mawasiliano ya simu ('mtumiaji mkuu' au 'mtumiaji mbadala'). Majibu kutoka kwa watumiaji wakuu na watumiaji mbadala yanalinganishwa/pirnia kwa uwiano asilia wa watumiaji wakuu na watumiaji mbadala wa mtoe huduma huyo ili kukokotoa NPS.

Mapato

Mapato ya huduma yalipungua kwa 1.0% hadi shilingi bilioni 956.5 ikichangiwa na athari za moja kwa moja, na zisizo za moja kwa moja za tozo ya serikali kwenye miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu za kiganjani, pamoa na shinikizo la ushindani. Athari za mashinikizo haya zinaakisiva na kupungua kwa matumizi ya wastani kwa mteja (ARPU) kwa 3.5% (ongezeko la 7.9%). Tukiondoa athari za tozo katika miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu za kiganjani, zinazokadirwa kuwa shilingi bilioni 103.8, mapato yetu ya huduma yaliongezekwa kwa 9.8%*, yakichochewa na uhitaji endelevu wa huduma zetu za kifedha, kidigitali na data. Kwa upande mwininge, idadi ya wateja wetu iliongezekwa kwa 3.4% hadi kufikia milioni 15.4, ikiakisi mafanikio ya utekelezaji wa mikakati ya kibashara yetu katika kuchochea ongezeko la idadi ya siku ambazo wateja wanatumia huduma zetu, na ongezeko la jumla la utumiaji wa huduma zetu.

Mapato ya huduma za simu kwa sauti yalipungua kwa 5.0% hadi shilingi bilioni 287.0, huku mchango wake kwenye mapato ya huduma ukipungua kwa alama za asilimia 1.3 hadi 30.0%. Sababu za msingi ya kupungua kwa mapato, ni kufungiwa huduma kwa wateja 568 000 ambao hawakawa wamekamiliwa usajili kwa njia ya alama za vidole (kibaiometriki), pamoa na shinikizo kubwa la ushindani wa bei liliatosababisha mporomoko wa 15.1% kwa bei ya wastani kwa dakika, huku idadi ya dakika zilizotumika ziliongezekwa kwa 10.0%.

Mapato ya M-Pesa yalipungua kwa 7.6% hadi shilingi bilioni 329.6. Tukiondoa athari za tozo kwenye miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu za kiganjani, mapato ya huduma ya M-Pesa yaliongezekwa kwa 17.7%*, yakichochewa na kukua kwa wigo wa huduma za M-Pesa, na ongezeko la utumiaji wa huduma. Bidhaa yetu ya mkopo 'Songesha,' imeedeleta kufanya vizuri katika kuwesheza ukamilishaji wa miamala ya wateja. Mapato ya Songesha yameongezeka kwa 22.7%, na kuongeza mchango wake katika mapato ya jumla ya M-Pesa kwa alama za asilimia 1.8 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Tunafuraha kwamba, licha ya kuwepo changamoto zilizotokana na tozo kwenye miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu za kiganjani, tumeendelea kuwawezesha wateja na mawakala wetu, kutatua mahitaji yao ya kifedha ya muda mfupi, kupitia huduma zetu za mikopo ya Songesha, M-Pawa na mikopo ya muda mfupi kwa mawakala. Mwaka huu, mikopo na ovadrafiti yenye thamani ya shilingi bilioni 562.4 ilitolewa kwa mawakala na wateja wetu, ikiwa ni ongezeko la karibu 40% ikilinganishwa na mwaka uliopita. Hii ni katika kutimiza azma yetu, ya kuchangia na kuunga mkono huduma jumuishi za kifedha.

Huduma yetu ya 'Lipa kwa Simu', ambayo inawapatia wateja uwezo wa kukamilisha malipo ya manunuzi, imeedeleta kukua. Mwaka huu zaidi ya wateja milioni moja, walifanya miamala yenye thamani ya zaidi ya shilingi trillioni 1.7 katika mfumo huu wa malipo, ikiwa ni ongezeko la zaidi ya 25% kwa mwaka. Ukuaji huu ni uthibitisho wa mafanikio yetu katika kuchochea matumizi, na kuongeza huduma katika mfumo wa M-Pesa. Na muhimu zaidi, kuwapatia wateja wetu huduma za kiteknolojia zinazo tattu changamoto na kurahisisha utekelezaji wa miamala mbalimbali.

Huduma yetu ya uhamishaji fedha kimataifa pia imeedeleta kutoa mchango muhimu katika kuongeza ujumuishi wa kifedha, kukiwa na miamala yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 850, ambayo ni ongezeko la zaidi ya 40%, iliyofanyika katika mwaka huu. Kwa ujumla, mfumo wetu wa M-Pesa ulikamilishwa miamala yenye thamani ya zaidi ya shilingi trillioni 60, ikiwa ni upungufu wa 11% ikilinganishwa na mwaka uliopita, ikidihirisha ukubwa wa athari za tozo kwenye miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa simu za kiganjani, licha ya punguza la tozo kwa 30%, litilotolewa na serikali mwezi Septemba 2021. Thamani ya miamala kwenye huduma - msingi ya kutuma pesa katika mteja na mteja, ilipungua kwa takribani 40% baada ya utekelezaji wa tozo na kuathiri hatua tuliyokuwa tumekwisha ipiga katika kuongeza ujumuishi wa kifedha nchini kuitopia huduma ya M-Pesa. Jambo la kutia moyo, ni kwamba mapato ya huduma zetu mpya za kibunifi ya mameithibitika kuwa thabiti zaidi dhidi ya athari za tozo. Mapato kutohata na huduma zetu za mikopo yaliongezekwa kwa 26.1% yakilinganishwa na mwaka uliopita, yakichochewa na ongezeko la utumiaji endelevu wa huduma hizo.

Mapato ya huduma ya data yaliongezekwa kwa 18.9% kufikia shilingi bilioni 204.0. Kimsingi, ongezeko likitokana na kukua kwa 20.3% katika wastani wa mapato kwa mtumiaji wa data, kutohata na kuendelea kuongeza kwa uhitaji wa huduma za data. Matumizi ya jumla ya data yaliongezekwa kwa 20.8%, yakichangiwa na kuongeza kwa simu janja mtandaoni. Watumiaji wa simu janja waliongezekwa kwa 12.1% hadi wateja milioni 4.1 ikiwa ni sawa na 54.2% ya wateja wetu wa data, kiasi ambacho ni ongezeko la alama za asilimia 13.5 ukilinganishwa na mwaka uliopita. Ongezeko la simu janja lilichangia kukua kwa

matumizi ya wastani ya data kwa mteja kufikia gigabaiti 1.7 kwa mteja - kwa mwezi, ongezeko la 22.3% ukilinganishwa na mwaka uliopita. Huduma ya data inaendelea kuwa huduma muhimu katika kukuza mapato na pia kutekeleza azma yetu ya kuunganisha watu kwa kesho iliyo bora. Na ndio maana tumeendelea kuchukua hatua kuhamasisha ongezeko la utumiaji na watumiaji wa data ikiwa ni pamoa na kujenga minara mipy 143 ya 4G, mbali na minara mingine zaidi ya 530 nchi nzima, ambayo iliongezwa uwezo, kwa lengo la kuboresha huduma kwa wateja.

Mapato ya huduma za kidigitali na huduma za ziada, yanayojumuisha mapato ya mkopo wa muda wa hewani – Nipige tafu, na mapato ya huduma za ziada – 'VAS', yaliongezekwa kwa 46.6% hadi shilingi bilioni 36.3, kimsingi, yakichochewa na ongezeko la 48.4% kwenye matumizi ya wastani kwa mteja. Ongezeko hili linaonesha mafanikio ya utekelezaji wa mikakati ya kibashara katika kuongeza wigo wa huduma zetu za kidigitali na huduma za ziada, kwa lengo la kuongeza idadi ya wateja wanaotumia huduma hizo, na kuchochea uhitaji wake.

Mapato ya simu zinazoingia yalipungua kwa 17.3% hadi shilingi bilioni 48.1 yakichangiwa na kupungua kwa 41.9% kwa wastani wa mapato kwa dakika, kwa simu zinazoingia kutoka mitandao mingine, ikichagizwa na kushushwa kwa 'gharama zinazo toza kwa dakika, kwa simu zinazoingia kutoka mitandao mingine' – MTR, kutoka shilingi 5.2 hadi shilingi 2.6 mnamo Januari 2021 na tena kupunguza kufikia shilingi 2.0 mnamo Januari 2022, kadri ya muongozo wa TCRA. Kupungua kwa viwango vya kuunganisha mitandao mingine kulifidiwa kwa kiasi, na ongezeko la 42.4%, kwenye dakika za simu zilizopokelewa kutoka mitandao mingine, kutokana na ushindani wa soko uliochochea watoa huduma kutekeleza kuongeza idadi ya dakika wanazota katika vifurushi.

Mapato ya ujumbe mfupi wa maneno yalipungua kwa 9.5% hadi shilingi bilioni 28.9 ikichangiwa na kupungua kwa idadi ya jumbe zilizotumwa.

Gharama¹

Gharama ziliongezekwa kwa 1.4% (ongezeko la 8.2%*) hadi shilingi bilioni 670.4. Jitihada zetu za kufanya mabadiliko katika matumizi zilikuwa na mafanikio, na ziliookoa matumizi yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 40. Japokuwa gharama za moja kwa moja zilipungua kwa 0.8%, ikichangiwa na kupungua kwa mapato, shinikizo la ushindani lisilasababisha ongezeko la gharama za kamisheni kwa mawakala, na vilevile ongezeko kwenye gharama za kuunganisha simu kwenda mitandao mingine. Gharama zilizookolewa kutokana na juhudhi za kudhibiti matumizi, zilifidiwa na shinikizo la gharama zinazohusiana na wafanyakazi na matumizi ya uendeshaji. Gharama za wafanyakazi ziliongezekwa kwa 3.6%. Iwapo tukiondoa athari ya upungufu wa gharama usiojurudia, uliofanayika mwaka uliotangulia, gharama za wafanyakazi zilipungua kwa 2.8%, ikiwa ni matokeo chanya ya marekebisho iliyofanyika katika uendeshaji biashara. Gharama nyininge za uendeshaji ziliongezekwa kwa 7.5% zikichangiwa na malipo ya kodi zinazohusiana na makadirio ya ushuru wa 'excise' wa miaka iliyopita, ongezeko la ada za kisheria zinazohusiana na usuluhishi wa kesi mbalimbali za kodi, na vilevile ongezeko la gharama za mtandao kutokana na ongezeko la ukubwa wa mtandao kufuata uwekezaji unaoendelea na pia marekebisho ya mfumuko wa bei kadri ya mikataba iliyopo ya huduma. Ukitoa gharama zisizojrudia, gharama nyininge za uendeshaji ziliongezekwa kwa 2.1% tu, zikiakisi hatua madhubuti za kupunguza gharama zilizochukuliwa mwaka huo.

'EBITDA'

Mapato kabla ya riba, kodi na gharama za uchakavu, yalipungua kwa 5.0% hadi shilingi bilioni 300.3 yakiatirisha na athari za tozo kwenye miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa simu za kiganjani. Tukiondoa athari za tozo zinazokadirwa kufikia shilingi bilioni 59.1, mwaka huu 'EBITDA' iliongezekwa kwa 13.7%*, ikiwa ni sawa na 33.4% ya mapato yote, ongezeko la alama ya asilimia 1.0. Ufanisi huu unachangiwa na ukuaji wa mapato ya huduma na hatua za kudhibiti ongezeko la matumizi.

Gharama za uwekezaji

Katika mwaka ulioisha wa fedha, tuliwekeza kiasi cha shilingi bilioni 173.9, ikiwa ni sawa na 17.9% ya mapato yetu, kwa lengo la kuendelea kuongeza ubora wa mtandao wetu, kupuanu wigo wa eneo la upatikanaji wa huduma, na kuboresha miundombini ya TEHAMA. Ongezeko la minara mipy 143 ya 4G mwaka huo, ili kuongeza uwezo na wigo wa upatikanaji wa mtandao wetu wa 4G, vilichangia katika kukua kwa 59.0% katika matumizi ya data yaliyopitia mtandao wa 4G, na pia kupata alama cubwa ya uongozi wa 'Net Promoter Score' kwenye ubora wa mtandao, tukiwa na alama 14 zaidi ya mshindani anayetufuati katika nafasi ya pilii.

1. Gharama mbali na gharama za uchakavu.

Muhtasari wa taarifa za pamoja za hali ya kifedha

Shilingi (milioni)	Zimekaguliwa 2022	Zimekaguliwa 2021	
Mapato	971 025	974 391	Mapato yamepungua kwa 0.3% hadi shilingi bilioni 971.0 yakichangiwa na kupungua kwa 1.0% katika mapato ya huduma kulikochochewa na athari za moja kwa moja, na zisizo za moja kwa moja za tozo kwene miamaala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa simu za kiganjani, shinikizo kubwa la ushindani hususani katika bei za huduma ya simu kwa sauti, pamoja na kupungua kwa mapato ya simu zinazoingia kutoka mtandao mingine, kutokana na kupunguzwa kwa 23.1%, kwa gharama inayo tozwa kwa kila dakika ya simu inayotoka mtandao mingine kadiri ya kanuni za TCRA. Athari hizi zimesababisha kupungua kwa 3.5% (ongezeko la 7.9%*), kwa wastani wa matumizi kwa kila mteja. Tukiondoa athari za tozo, zinazokadiriwa kuwa kiasi cha shilingi bilioni 103.8, mapato ya mwaka huu yaliongezeka kwa 10.3%*.
Gharama za moja kwa moja	(299 185)	(301 533)	
Gharama za wafanyakazi	(63 823)	(61 579)	
Gharama za Kujitangaza	(30 184)	(35 775)	
Gharama nyininge za uendeshaji	(279 472)	(260 064)	
Gharama za uchakavu	(236 201)	(264 039)	
Gharama za madeni chechefu	2 275	(1 887)	
Faida ya uendeshaji	64 435	49 514	Gharama zilongezeka kwa 1.4% (ongezeko la 8.2%*) hadi TZS bilioni 670.4. Ongezeko hili lirmechangiwa na gharama ndogo zinazohusiana na wafanyakazi katika mwaka uliopita- zikichangiwa na upungu usiojirudia wa gharama, ongezeko la gharama katika kamisheni na gharama za kuunganishi mitandao ya simu zilizosababisha na shinikizo la ushindani wa soko, na vilevile ongezeko la gharama nyininge za mtandao - kimsingi kutokana na ongezeko la ukubwa wa mtandao kufuatia uwekezaji unoaindelea, na pia marekebisho ya mfumuko wa bei kadiri ya mikataba iliyopo ya huduma. Hattua tulizo zitekeleza katika kudhibiti matumizi, zilikuwa na mafanikio, zikiokoa matumizi ya zaidi ya shilingi bilioni 40, ambazo hata hivyo zilifidiwa na ongezeko katika gharama nyininge. Iwapo tukiondoa athari ya upungufu wa gharama zinazohusisa wafanyakazi, zisizojirudia uliofanyika mwaka uliopita, ambazo zinasababisha ongezeko la 3.6% iliyoripotiwa, Mwaka huu gharama za wafanyakazi zilipungua kwa 2.8%. Upungufu huu ni matokeo chanya ya marekebisho yaliyofanyika katika uendeshaji biashara. Gharama nyininge za uendeshaji zilongezeka kwa 7.5%, zikichangiwa na malipo ya kodi zinazohusiana na makadirio ya ushuru wa 'excise' wa miaka iliyopita, ongezeko la ada za kisheria zinazohusiana na usuluhishi wa kesi mbalimbali za kodi, na vilevile ongezeko la gharama za mtandao kutokana na ongezeko la ukubwa wa mtandao kufuatia uwekezaji unoaindelea, na pia marekebisho ya mfumuko wa bei kadiri ya mikataba iliyopo ya huduma. Ukitoa gharama zisizojirudia, gharama nyininge za uendeshaji zilongezeka kwa 2.1% tu, zikiakisi hattua madhubutu za kupungua gharama zilizochukuliwa mwaka huo.
Mapato ya kifedha	25 837	38 418	
Gharama za kifedha	(85 544)	(85 232)	
(Hasara)/mapato kutokana na mabadiliko ya viwango vya kubadili fedha za kigeni	(1 548)	3 627	
Faida kabla ya kodi	3 180	6 327	Gharama za uchakavu zilipungua kwa 10.5% ikiwa ni matokeo ya mapitio ya umri na muda ambapo mali (assets) zinaweza kuendelea kutumika kwa ufanisi. Upungufu ulifididiwa kwa kiasi na ongezeko kutokana na uwekezaji impya katika mali. Mapitio haya ya mali yaliyofanyika kulingana na sera za kampuni.
Gharama za kodi ya mapato	(23 443)	(36 433)	
(Hasara) kwa mwaka	(20 263)	(30 106)	Gharama za madeni chechefu zinahusisha kiasi kilichotengwa kwa ajili ya hasara tarajiva za madeni chechefu, tunayowadai wateja na washirika wetu kibashara. Madeni ya biashara huripotwa katika kiasi halisi cha deni, kikipunguzwa na kiasi cha hasara tarajiva cha madeni hayo, kwa mujibu wa tathmini ya menejimenti juu ya uwezo wa wadeni kurejesha mikopo hiyo. Madeni yote hupimwa ili kutathmini uwezekano wake wa kutokulipa. Gharama kutokana na madeni chechefu zimepungua kutokana na kuimarka kwa makusanyo katika huduma ya mikopo ya muda wa maongezi (Nipige tafu).
Mapato mengine	—	—	
Jumla ya hasara halisi kwa mwaka wa mapato, baada ya kutoa kodi¹	(20 263)	(30 106)	Mapato ya kifedha yamepungua kwa 32.7%, kutokana na kupungua kwa uwekezaji katika hati fungani za serikali kufuatia kulipa gawio maalum katika nusu ya pili ya mwaka uliotangulia, na pia viwango vidogo vya riba vilivypokolewa kwa akiba za fedha taslimu.
(hasara) ya msingi na mchanganyiko kwa kwa kila hisa (shilingi)	(9.05)	(13.44)	Hasara kutokana na mabadiliko ya viwango vya kubadili fedha za kigeni inatokana na kubadilika kwa viwango vya kubadili fedha za kigeni na kusababisha hasara ya shilingi bilioni 1.5 kwa akiba ya fedha za kigeni tulizonazo, ikiltinganishwa na mwaka uliopita, ambapo tulipata faida.

1. Mapato yote yahawahu wamiliki wa Kampuni mama, kwa kuwa hakuna wamiliki walio na umiliki mdogo kwenye Kampuni tanzu.

Muhtasari wa taarifa za pamoja za hali ya kifedha

Shilingi (milioni)	Zimekaguliwa 2022	Zimekaguliwa 2021	
MALI			
Mali za kudumu	1 191 715	1 219 874	Kupungua kwa mali na mitambo kumetokana na gharama za uchakavu zikifidiwa kwa kiasi na uwekezaji uliofanyika mwaka huu.
Mali na mitambo	1 014 626	1 041 226	Kuongezeka kumetokana na uwekezaji mwaka huu, ukifidiwa kwa kiasi na gharama za uchakavu.
Mali zisizoshikika	76 681	70 593	Kupungua kumetokana na gharama za uchakavu na haki iliyohamishwa kwenda katika haki za muda mfupi, zikifidiwa kwa kiasi na uwekezaji uliofanyika mwaka huu.
Malipo ya 'Haki ya matumizi' kabla ya kutumia Thamani isiyoshikika ya uwekezaji	44 582	46 559	Ongezeko limechochewa na malipo ya kodi ya utangulizi yaliyolipwa dhidi ya hati za madai ya kodi zilizopokelewa mwaka huu, ikifidiwa kwa kiasi, na kiasi kilichohusika na dai la 'Transfer pricing' la miaka iliyopita ambalo limehamishwa na kurekodiwa kwenye gharama.
Kodi ya mapato inayotarajiwa kurejeshwa	1 639	1 639	
Madeni ya kibiashara na madeni mengine	41 011	39 772	
Kodi iliyoahirishwa	11 388	18 696	Upungufu umetokana na kurekodiwa kwenye gharama kwa madai yaliyokuwa yanahusiana na tozo ya 'excise' kwenye mapato yanayotokana na matumizi ya wateja kutoka mitandao ya nje ya nchi na simu zilizopokelewa kutoka nchi za nje.
Mali za muda mfupi	1 788	1 389	
Malipo ya 'Haki ya matumizi' kabla ya kutumia	846 914	836 067	Ongezeko limetokana na malipo yaliyolipwa kwa utangulizi katika kipindi cha mwaka huu, yakifidiwa kwa kiasi na malipo yaliyohamishwa kwenda katika maliopo ya utangulizi ya muda mfupi.
Mali ghalani	15 864	13 188	
Madeni ya kibiashara na madeni mengine ya kulipwa	2 597	4 179	Upungufu unatokana na kuuzwa kwa simu na vifaa, ukifidiwa kwa kiasi na simu na vifaa vlivyopokelewa mwaka huu.
Kodi ya mapato inayotarajiwa kurejeshwa	112 570	125 534	
Rasilimali za kifedha – M-Pesa	22 836	4 726	Upungufu unatokana na ufanisi katika ukusanyaji wa madeni kwa wabia wa kibiashara pamoja na madeni ya mikopo ya muda wa hewani (Nipige tafu).
Fedha taslimu na mbadala wa fedha	436 086	444 183	
JUMLA YA MALI	256 961	244 257	
	2 038 629	2 055 941	
Mtaji na Madeni	777 324	797 587	
Mtaji wa hisa	112 000	112 000	
Malipo ziada kwenye hisa	442 435	442 435	
Mchango wa mtaji	27 698	27 698	
Ziada ya faida iliyotunzwa	195 191	215 454	
Madeni ya muda mrefu	451 764	466 184	
Madeni ya pango	446 044	461 627	Ongezeko limetokana na kufikiwa maamuzi kwa baadhi ya majadiliano juu ya migogoro ya kodi ya mapato kwa kipindi cha mwaka 2015 -2020, yakifidiwa kwa kiasi na kutambuliwa kwa gharama kuhusiana na dai la 'Transfer pricing' la miaka iliyopita.
Ruzuku za serikali	143	235	
Madeni ya kibiashara na madeni mengine ya kulipa	378	163	Upungufu unaakisi athari za tozo kwenye amana za wateja binafsi na wa biashara wa M-Pesa.
Tahadhari ya madeni	5 199	4 159	
Madeni ya muda mfupi	809 541	792 170	Ongezeko linatokana na kuongezeka kwa fedha taslimu kutokana na uendeshaji wa biashara.
Madeni ya pango	60 472	73 052	Upungufu unatokana na hasara kwenye uendeshaji biashara, hasa ukiakisi athari za tozo kwenye miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu za kiganjani.
Madeni ya biashara na mengine ya kulipa	300 006	253 153	
Madeni ya biashara yanayohusu M-Pesa	436 086	444 183	Madeni yamepungua kutokana na kulipa madeni ya pango yaliyoiva kwenye mikataba ya 'haki ya matumizi', na kuhamishwa kwenda kwenye "haki ya matumizi" ya muda mfupi kwa madeni yanayokaribia kuiva.
Ruzuku za serikali	1 218	1 383	
Tahadhari ya madeni	11 759	20 399	Upungufu unatokana na kulipa kwa madeni yaliyoiva. Ukipidiwa kwa kiasi na ongezeko kutokana na mikataba mipy, ongezeko la riba na ongezeko la gharama kadiri ya mikataba.
Jumla ya madeni	1 261 305	1 258 354	
JUMLA YA MTAJI NA MADENI	2 038 629	2 055 941	
Upungufu umechangiwa kwa kiasi kikubwa na ulipwaji wa madeni ya matangazo kwa halmashauri za manipaa baada ya kukamilika kwa zoezi la kulinganisha madeni (reconciliation).			
Upungufu unatokana na kupungua kwa amana za wateja wa M-Pesa kutokana na athari za tozo kwenye miamala ya kuhamisha na kutoa fedha kwa njia ya simu za kiganjani.			
Ongezeko limechangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko mahususi la uwekezaji katika mtandao katika kipindi kuelekeea mwishoni mwa mwaka.			

Muhtasari wa taarifa za pamoja za mzunguko wa fedha

Shilingi (milioni)	Zimekaguliwa 2022	Zimekaguliwa 2021	
Fedha zilozalishwa kutokana na uendeshaji	316 748	427 135	Upungufu unatokana hasa na malipo kwa wadeni wetu, yakifidiwa kwa kiasi na kuongezeka kwa ukusanyaji wa madeni ya mawakala na wateja walikopa muda wa hewani – Nipige Taifu.
Malipo ya kodi ya mapato	(43 191)	(67 642)	
Riba kwenye malipo ya kodi	(5 753)	–	
Mzunguko ghafi wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji	267 804	359 493	Upungufu unatokana na kupungua kwa faida ya kampuni ya M-Pesa limited kutokana na athari za tozo.
Mzunguko wa fedha zilizotumika katika shughuli za uwekezaji			Hii ni kutokana na madeni ya kodi ya miaka iliyopita yaliyolipwa baada ya kukamilika kwa majadiliano.
Nyongeza katika mali na mitambo, na mali zisizoshikika	(142 153)	(112 850)	Ongezeko ni kadiri ya uwekezaji katika mtandao na TEHAMA, uliopitishwa kwa kipindi cha mwaka, pamoja na uwekezaji maalum.
Mapato kutokana na mauzo ya mali na mitambo	6	17	
Ruzuku za serikali zilizopokelewa	4 991	400	
Marejesho ya uwekezaji wa muda mfupi	–	164 643	
Mapato ya fedha yaliyopokelewa	7 219	17 625	Ongezeko limetokana na kulipwa kwa ruzuku kutoka UCSAF kwa miradi iliyokamilika.
(Kuongezeka)/Kupungua kwa fedha zilizowekwa kwenye akiba za matumizi maalum	8 097	(106 627)	Upungufu umetokana na kutowekeza tena katika hawala za serikali baada ya zilizokuwepo kuiva.
Riba kutoka amana za M-Pesa	18 618	20 793	Upungufu umetokana na kupungua uwekezaji katika hawala za fedha, kama ilivyoolezewa hapo juu.
Mzunguko halisi wa fedha katika shughuli za uwekezaji	(103 222)	(15 999)	Upungufu umetokana na kupungua kwa amana za wateja wa M-Pesa, kutokana kupungua kwa matumizi kulikosababishwa na Tozo kwenye miamala ya fedha.
Gawio tulitolipa	(209)	(427 093)	Upungufu ni kutokana na kupungua kwa amana za M-Pesa limited kutokana na kupungua kwa amana za wateja wake kama ilivyoolezewa hapo juu.
Riba ya madeni ya pango iliyolipwa	(60 871)	(64 040)	Upungufu umetokana na kupungua kwa amana za wateja wa M-Pesa, kutokana kupungua kwa matumizi kulikosababishwa na Tozo kwenye miamala ya fedha.
Malipo ya madeni ya pango – mtaji	(69 183)	(61 395)	Upungufu ni kutokana na kupungua kwa amana za M-Pesa limited kutokana na kupungua kwa amana za wateja wake kama ilivyoolezewa hapo juu.
Riba iliyolipwa kwa wateja wa M-Pesa	(20 043)	(24 165)	Upungufu umetokana na kupungua kwa amana za wateja wa M-Pesa, kutokana kupungua kwa matumizi kulikosababishwa na Tozo kwenye miamala ya fedha.
Mzunguko halisi wa fedha zilizotumiwa katika shughuli za ugharimiaji	(150 306)	(576 693)	Upungufu ni kutokana na kupungua kwa amana za M-Pesa limited kutokana na kupungua kwa amana za wateja wake kama ilivyoolezewa hapo juu.
Ongezeko/(punguzo) ghafi katika fedha na fedha mbadala	14 276	(233 199)	Upungufu umetokana na kupungua kwa amana za wateja wa M-Pesa, kutokana kupungua kwa matumizi kulikosababishwa na Tozo kwenye miamala ya fedha.
Fedha taslimu na fedha mbadala tarehe 1 Aprili	244 257	473 828	Upungufu umetokana na kupungua kwa amana za wateja wa M-Pesa, kutokana kupungua kwa matumizi kulikosababishwa na Tozo kwenye miamala ya fedha.
Athari za mabadiliko ya viwango vya kubadili fedha katika fedha taslimu na fedha mbadala zilizo katika fedha za kigeni	(1 572)	3 628	Upungufu umetokana na kupungua kwa amana za wateja wa M-Pesa, kutokana kupungua kwa matumizi kulikosababishwa na Tozo kwenye miamala ya fedha.
Fedha taslimu na fedha mbadala kufika tarehe 31 Machi	256 961	244 257	Ongezeko limetokana na ongezeko la mikataba ya pango iliyoviwa.
			Upungufu ni kutokana na kupungua kwa riba kutokana na uwekezaji wa fedha za M-Pesa limited kutokana na kupungua kwa amana za wateja wake kama ilivyoolezewa hapo juu.



Taarifa ya Wajibu wa Shirika kwa Jamii (CSR)

Tukiwa tunaongozwa na malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (UN-SDGs), Dira ya Tanzania 2025 na Mpango wake wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano, dira ya wajibu wa Kampuni kwa Jamii ya Vodacom Tanzania ni kuleta mabadiliko chanya kwenye maisha ya watu waliokekwa pembezoni katika jamii za Kitanzania, tukitumia uwezo wa Kampuni kiteknolojia na fursa za ubia katika kutekeleza miradi ya afya ya kina mama, elimu na ulinzi wa mazingira.

Tangu 2004, Vodacom Tanzania kupitia kurugenzi ya Mahusiano ya Shirika¹, imewekeza moja kwa moja zaidi ya shilingi bilioni 16.9 katika kubadili maisha ya mamilioni ya watu nchini Tanzania, kupitia programu mbalimbali za wajibu wa shirika kwa jamii. Uwekezaji uliotajwa hapa, haujumuisha takwimu za fedha taslimu na mali zilizowekezwa katika programu mbalimbali na washirika wetu, Vodafone Foundation – 'Mfuko wa kijamii wa Kampuni mama'.

Mafanikio yetu 2022

Afya – Lengo la 3 la Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu

(Afya njema na ustawi)

Programu yetu ya M-Mama inayotekelzeza kwa kushirikiana na Mfuko mama - Vodafone Foundation, inatoa huduma ya usafiri wa dharura kwa wanawake wajawazito. Lengo likiwa ni kusaidia kuzuia na kupunguza vifo vya kina mama na watoto. Tangu kuanzishwa kwake kwa majaribio mwaka 2013, programu hii imewanufaisha walengwa zaidi ya 12 000 ikijumuisha wanawake na watoto wachanga katika maeneno ya Kanda ya ziwa ya Mwanza na Shinyanga. Katika programu hii, tunatumia huduma ya M-Pesa kulipia huduma za 'teksi jamii' zilizosajiliwa, ambazo zinatumika kama mbadala wa magari ya wagonjwa. Kudhihirisha umuhimu wa huduma hii, toka mradi uanzishwe, 20% ya matukio ya dharura yaliyotokeza, yalihudumiwa na magari ya wagonjwa ya serikali na 80% iliyobaki ikifanywa na teksi -jamii. Pia mradi umewapatia mafunzo zaidi ya wafanyakazi 300 wa sekta ya afya na madereva 200 wanaoshiriki katika programu hii kama sehemu ya programu, ambayo ni faida ya ziada kwa jamii. Mnamo Aprili 2022, program ilizinduliwa rasmi kuhudumia watu wengi zaidi, kwa ushirikiano na serikali katika jithida za kupunguza vifo vya kina mama. Mradi uliozinduliwa, utahudumia kina mama na watoto katika mikoa 14, yenyé takribani 50% ya watu wote nchini. Mfuko jamii wa kampuni mama ya 'Vodafone foundation' umeahidi kuwekeza kiasi cha dola za marekani milioni 9.3 katika awamu hii ya programu itakayochukua miaka sita.

Pia, katika kusaidia kutoa huduma ya afya kwa watoto, mwaka huu tumechangia vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 58.4 kuhudumia kitengo cha huduma ya watoto waliozaliwa kabla ya wakati (njiti) na kitengo cha kina mama wajawazito katika hospitali ya Mkomaindo huko Masasi, mkoani Mtwara. Vifaa viliviyotolewa vinajumuisha vitanda vya kujifungulia, vifaa vya msaada wa kuvuta hewa, mitungi ya Oksijeni, mashine ndogo ya Ultrasound, seti za kujifungulia, mashine za kupima shinikizo la damu, kifaa cha joto kwa watoto, kifaa cha kupima kiasi cha oksijeni mwilini na vifaa vingine vingi.

1. Masuala ya Uwajibikaji wa Kampuni kwa jamii yaliyokuwa yanasisimamiwa na Mfuko wa 'Vodafone Foundation', kwa sasa yanasisimamiwa na idara ya Mahusiano ya kampuni kufuatia kufungwa kwa hiari kwa mfuko wa 'Vodafone Foundation'.



Tumeendelea kuiunga mkono Wizara inayohusika na masuala ya Afya katika jithida za kutoa huduma za afya kidigitali inayotolewa katika mfumo wa wizara 'mHealth technical platform' kupitia ujumbe mfupi wa maneno kwa kutumia namba ya USSD *152*05# na SMS kwenda 15 205. Mfumo wa 'mHealth' umesajili zaidi ya watumiaji milioni 3 kutoka katika mitandao yote ya simu za kiganjani nchini, zinazofanya kazi tangu ulipozinduliwa mwaka 2012, ambapo takribani wasajiliwa milioni 1.5 ni watejda wa Vodacom, ambao kwa kipindi hicho, wamepata zaidi ya jumbe fupi milioni 100 bure, zenyé habari muhimu kuhusu masuala ya afya, na hivyo kuchangia katika kulinda uhai. Pia tunaipatia Wizara ya Afya huduma ya bure ya kutumia USSD, ambayo inawawezesha wafanyakazi wa sekta ya afya na wanajamii kupata huduma za mHealth kama vile Mfumo wa Utafiti na Kushughulikia Magonjwa Kielektroniki (e-IDSR) na mfumo kwa ajili ya kutoa maoni na mrejesho kwa Wizara ya Afya.

Pia tunatoa huduma ya kupiga simu bure kwenda kituo cha msaada cha Wizara ya Afya 'Afya Call Centre' inayopatikana kwa kupiga simu namba 199. Kituo hiki, kinawezesha upatikanaji wa taarifa ya huduma mbalimbali za afya kwa magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza ikijumuisha UVIKO-19 na VVU. Kwa wastani, zaidi ya dakika 100 000 za bure hupigwa kwenda namba hii ya simu kila mwezi.

Pia tumeiunga mkono Wizara ya Afya katika maeneo ya kujenga uwezo na marekebisho ya sera. Mwaka huu tumetumia shilingi milioni 38.3 kugharamia warsha za kupitia sera na uhamasishaji, kwa lengo la kuingiza ajenda ya matibabu ya watoto njiti katika mipango ya kitaifa. Lengo likiwa kuiomba serikali ya Tanzania, kupitia Wizara ya Afya, kurekebisha sheria, kanuni na sera zinazohusu likizo ya wazazi waliopata watoto njiti, kuingiza gharama za matibabu na uangalizi wa watoto waliozaliwa kabla ya wakati katika vifurushi vya bima ya afya, na kuingiza mafunzo kuhusu masuala ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati katika mifumo na mitaala ya sasa ya elimu Tanzania.

Elimu – Lengo la 4 la Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu
(Elimu Bora)



Matumizi ya jumla ya zaidi ya shilingi
milioni 758.8

kwa mwaka.

Tumeendelea kutoa msaada katika jitihada mbalimbali za kielimu nchini, kwa kushirikiana na mfuko mama wa Vodafone foundation, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji na Wizara ya Sayansi na Teknolojia, na vilevile mashirika na asasi mbalimbali zisizo za kiserikali ikijumuisha 'The African Child Projects'.

Programu yetu ya 'Instant Schools', ambayo inalenga jamii za pembezoni za vijiji ni katika mikoa mbalimbali nchini Tanzania, inatoa huduma ya elimu bure kwa wanufaika zaidi 185 000 waliosajiliwa kuitia mfumo wetu wa mtandaoni wa E-Fahamu. Mfumo huu unawapa watumiaji uwezo wa kusoma vitabu mtandaoni, na unafikiwa na wateja wetu kuitia simu janja au kompyuta. Kwa sasa huduma hii inatoa masomo bure kwa wanafunzi zaidi ya 81 000 wa shule za msingi na sekondari nchini. Huduma hii inachochewa na programu yetu ya 'Shule Janja' (Smart schools) ambayo inatoa kompyuta, viunganishi vya intaneti – 'routers' na mtandao wa intaneti bure kwa zaidi ya shule 500 za msingi na sekondari katika jamii nchini, ambazo kwa mazingira yake, bila msaada, zingebaki bila kuunganishwa kintandao.

Pia kwa kushirikiana na idara yetu ya rasilimali watu, mwaka huu, kuitia programu yetu ya #Codelikeagirl, tumewasaidia wasichana 306 wenye umri kati ya miaka 14-18, kujenga ujuzi wa TEHAMA na stadi muhimu za maisha na kuwashimiza kufikiri kuchukua masomo ya TEHAMA, sayansi na hesabu 'STEM'.

 Maeleo mengine kuhusu programu hii yanapatikana katika **Ukurasa wa 16**

Ulinzi wa mazingira – Lengo la 13 la Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu
(Kuchukua Hatua za Kulinda Mazingira)



Tumetumia zaidi ya shilingi
milioni 104.5

mwaka huu'.

Tangu mwaka 2020, kuitia iliyokuwa 'Vodacom Foundation', kwa kushirikiana na World Wide Fund for Nature (WWF) na Halmashauri ya Jiji la Dodoma, tumeekuwa tukitekeleza kwa pamoja programu ya 'Kijanisha Dodoma' na programu ya 'Kijani Zaidi', ikiwa ni jitihada za kupanda miti na kutoa elimu ili kufanya mji mkuu wa Tanzania uwe wa kijani. Kwa sasa tuna miti 96 000 ilio hai chini ya mradi huu, na tumetumia zaidi ya shilingi milioni 410.5 katika mradi huu tangu ulipozinduliwa.

Programu zetu zinazohusiana na mazingira zimenufaisha jamii mbalimbali, si kwa miti iliyopandwa tu, bali pia kuitia programu za kujenga uwezo kwa zaidi ya wanajamii 800, ikiwa ni vikundi vya vijana na wanawake wajasiriamali. Mafunzo yanayotolewa ni pamoja na elimu kuhusu kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi, ikiwa ni pamoja na matumizi ya teknolojia endelevu kwa ajili ya shughuli za uzalishaji kiuchumi.

Pia tumeendelea kufanya kazi kwa ushirikiano na Mezzanine kuitia Kitengo chetu cha Biashara cha Vodacom katika mfumo wetu wa kidigitali wa M-Kulima ambao kwa sasa unawaunganisha zaidi ya wakulima wadogo 140 000 kwenye mnyororo wa thamani wa kilimo, kuwawezesha kupata taarifa, huduma na masoko kuitipa ujumbe mfupi wa maneno (SMS) na App, na ambao pia unawawezesha kupata malipo ya mauzo yao kwa haraka na usalama zaidi kuitia M-Pesa. Tunalengo la kuwa na wakulima milioni 1 katika mfumo huu kufika mwaka 2025, kuwasaidia kuongeza uzalishaji, mapato na uimara kiuchumi.

Lengo letu kimkakati

Katika miaka mitatu ijayo, tunalenga maeneo yafuatayo ili kuleta mabadiliko chanya kama njia ya kurudisha kwa jamii.

- **Kupunguza vifo vya watoto wachanga:** Tutasaidia utoaji wa vifaa ili kupunguza vifo vya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati - njiti, kujenga uwezo na kujenga ujuzi kwa wafanyakazi wa sekta ya afya wasio na ujuzi, na kuendelea kuchochlea ushirikiano wa sekta ya umma na sekta binafsi katika kupunguza kiwango cha vifo vya watoto wachanga. Tunaendeleza na azma yetu ya kufikia mikoa yote ya Tanzania na programu yetu ya M-mama kwa kushirikiana na mfuko mama wa Vodafone foundation, Serikali ya Tanzania kuitia Wizara zenye dhamana ya Afya, Serikali za Mitaa na Teknolojia ya Habari.
- **Kuunganisha Mtandao Vijijini:** kuendelea kutoa huduma ya mtandao katika jamii ambazo haza jangwa. Tunaamini kwamba kuziunganisha jamii za vijiji kwa mtandao ni muhimu katika kuondoa ombwe la kidigitali. Na hii itawezekana tu kwa kuwawezesha upatikanaji wa mawasiliano kwa gharama nafuu. Lengo hili ni sambamba na madhumuni yetu, ya kuhamasisha ujumuishi wa wote katika huduma za kidigitali.
- **Elimu jumuishi:** Tutahamasisha utoaji wa elimu jumuishi na kwa usawa kwa kuongeza upatikanaji wa teknolojia na mtandao wa intaneti katika shule za serikali nchini kote, kwa lengo la kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopata mafunzo kwa TEHAMA katika jamii zilizo katika mazingira magumu vijiji na mijini. Lengo letu ni kuzifikia shule 1 500 na kuwapatia fursa wanafunzi zaidi ya milioni moja kufika mwaka 2025.
- **Mabadiliko na tabianchi na bioanuwai:** Tutachochlea shughuli za kushughulikia mabadiliko ya tabianchi na upotevu wa bioanuwai nchini Tanzania, tukilenga kuzielimisha jamii kuhusu utunzaji wa mazingira, kuhimiza kilimo cha kisasa na kupanda miti, kuwawezesha upatikanaji wa nishati safi, na kusaidia uendeshaji wa makongamano kuhusu ajenda ya mabadiliko ya tabianchi.
- **Usimamizi wa shughuli za uokozu katika majanga:** Tutachochlea matumizi ya simu za kiganjani na Teknolojia ya TEHAMA kama zana za usimamizi wa majanga, tutatoa viunganishi vya intaneti – 'routers' na laini za simu kwa wadau watakaobainishwa, ili kuweza kuwaunganisha katika mtandao kwa ajili ya kusimamia majanga. Pia tutajikita katika kuwawezesha makongamano na semina kuhusiana na usimamizi wa majanga.
- **Kilimo cha kisasa na kupanda miti:** kuwawezesha upatikanaji wa nishati safi.

Viongozi wetu

Tuna Bodi yenyewe wakurugenzi 12, wengi wao ni wakurugenzi wasio watendaji. Mwenyekiti wetu ni mkurugenzi huru.

Muundo wa Bodi

Mwenyekiti



Thomas B Mihayo (75)

Aliteuliwa mwezi Novemba 2020

- Utaalamu wa Sheria.
- Msuluhihi.
- Mahusiano na serikali.

Wakurugenzi watendaji



Sitholizwe Mdlalose (42)

Mkurugenzi Mtendaji

Aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji mwezi Novemba 2021

- Kiongozi mwerevu wa biashara.
- Miaka 19 ya uzoefu katika usimamizi na ushauri wa fedha, ambapo 13 katika sekta ya mawasiliano ya simu katika masoko yanayoibukia.
- Utekelezaji madhubuti wa bidhaa za kibunifu na huduma mpya.



Hilda Bujiku (43)

Mkurugenzi wa Fedha

Aliteuliwa Mkurugenzi wa fedha mwezi Januari 2022

- Ujuzi mkubwa wa masuala ya fedha.
- Uzoefu mpana katika masoko yanayoibukia.

Wakurugenzi huru



Winifred Ouko (52)

Aliteuliwa mwezi Novemba 2017

- Utaalamu wa fedha na mipango.
- Uzoefu mpana wa uendeshaji na utekelezaji wa mikakati kimataifa.



Thembeka Semane (46)

Aliteuliwa mwezi Novemba 2017

- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika.
- Uzoefu katika utekelezaji wa shughuli za uendeshaji na mikakati.
- Utaalamu wa fedha.



Margaret Ikongo (65)

Aliteuliwa mwezi Novemba 2017

- Utaalamu wa fedha.
- Mahusiano na serikali.
- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika.

Wakurugenzi wasio watendaji



Diego Gutierrez (46)

Aliteuliwa mwezi Machi 2018

- Mpanga mikakati ya kibashara.
- Maarifa mapana kuhusu teknolojia ya simu na uzoefu wa masoko yanayoibukia.
- Utaalamu wa uongozi wa kimkakati.



Sudhersan Ramasamy (36)

Aliteuliwa mwezi Novemba 2021

- Utaalamu wa fedha na mipango.
- Uzoefu wa miaka 12 katika kundi la makampuni ya Vodafone.



Matimba Mbungela (50)

Aliteuliwa mwezi Agosti 2017

- Maarifa na uzoefu mpana wa usimamizi wa vipaji.
- Utaalamu katika taratibu bora za kusimamia rasilimali watu.
- Uzoefu katika uendeshaji wa shughuli za kimataifa.



Nkateko Nyoka (59)

Aliteuliwa mwezi Aprili 2020

- Uzoefu katika sheria na sera za umma.
- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika.
- Uongozi na mahusiano na wadau.



Dejan Kastelic (44)

Aliteuliwa mwezi Agosti 2020

- Uzoefu mpana wa sekta ya mawasiliano na TEHAMA.
- Uzoefu wa masoko mbalimbali ya kimataifa na yanayoibukia.
- Utaalamu wa uendeshaji na utekelezaji wa mikakati.



Raisibe Morathi (52)

Aliteuliwa mwezi Novemba 2020

- Uzoefu wa masuala ya fedha kimataifa.
- Utaalamu wa uongozi kimkakati.
- Utaalamu katika kung'amu fursa za kuunganisha au kununua biashara.

Kamati ya Utendaji



Sitholizwe Mdalose (42)

Mkurugenzi Mkuu

Alijiunga Vodacom
mwaka 2013, Vodafone
mwaka 2007



Hilda Bujiku (43)

Mkurugenzi wa Fedha

Alijiunga Vodacom
mwaka 2012



Linda Riwa (35)

Mkurugenzi wa Biashara –
Wateja Binafsi

Alijiunga Vodacom
mwaka 2017



Epimack Mbeteri (44)

Mkurugenzi wa Biashara
– M-Pesa

Alijiunga Vodacom
mwaka 2014



Arjun Dhillon (42)

Mkurugenzi wa Biashara –
Wateja wa Kibiashara

Alijiunga Vodacom
mwaka 2017, Safaricom
mwaka 2015



Andrew Lupembe (49)

Mkurugenzi Masuala ya
Mtandao

Alijiunga Vodacom
mwaka 2007



Olaf Mumburi (46)

Mkurugenzi wa Sheria na
Udhibiti

Alijiunga Vodacom
mwaka 2008



**Rosalynn Gloria
Mworia** (42)

Mkurugenzi Masuala ya
Mahusiano

Alijiunga Vodacom
mwaka 2008



**Harriet Atweza
Lwakatare** (44)

Mkurugenzi Huduma kwa
Wateja

Alijiunga Vodacom
mwaka 2012



Vivienne Penessis (47)

Mkurugenzi Rasilimali
Watu

Alijiunga Vodacom
mwaka 2018



Nguvu Kamando (47)

Mkurugenzi wa Huduma
za Kidigitali

Alijiunga Vodacom
mwaka 2002



Tax Agapinus (57)

Mkurugenzi Dharura na
Utekelezaji

Alijiunga Vodacom
mwaka 2020



Athumani Mlinga (54)

Mkurugenzi TEHAMA

Alijiunga Vodacom
mwaka 2003

Taarifa ya uongozi wa kampuni

Taarifa ya utekelezaji


Vodacom Tanzania Public Limited Company ('Vodacom Tanzania') inajizatiti kutoa huduma zenyenye ubora wa hali ya juu kwa uaminifu, maadili na utaalamu katika biashara.

Kanuni za uongozi wa kampuni zinajumuisha nidhamu, uhuru wa maamuzi, uwajibikaji, usawa, uwajibikaji kwa jamii, uwazi na uwajibikaji wa wakurugenzi kwa wadau.

Kanuni hizi zinazingatiwa katika taratibu za udhibiti wa ndani na sera za Vodacom Tanzania zinazoongoza utendaji wa kampuni na zinawiana na miongozo ya Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana kuhusu taratibu za usimamizi wa shirika unaofanywa na kampuni za umma zilizoorodheshwa nchini Tanzania.

Muundo wa usimamizi wa shirika

Muundo ufuatao unaonesha safu ya viongozi wa Vodacom Tanzania tarehe 31 Machi 2022:



Maadili ya viongozi

Bodi inakubali uwajibikaji wa pamoja katika kueleza namna ambavyo maadili na tabia za kimaadili zinapaswa kutekelezwa katika kampuni. Hii ni pamoja na kupanga taratibu za utendaji wa wajumbe wa bodi ili kuhakikisha kuwa wanatenda kwa uadilifu, uzoefu, uwajibikaji, haki na uwazi. Sifa hizi ni kipimo cha maadili kinachozingatiwa katika tamaduni za uendeshaji wa kampuni.

Uongozi na Kamati za Bodi

Bodi

Vodacom Tanzania ina bodi yenye wakurugenzi 12, ambapo kati yao wanenye (pamoja na Mwenyekiti) ni wakurugenzi huru wasio watendaji, sita kati yao si watendaji (lakini si huru kwa kuwa wanawakilisha wadau wakuu), na wawili ni wakurugenzi watendaji.

Bodi imeridhika kuwa uwiano wa wataalamu wenye maarifa, ujuzi na uzoefu wa aina mbalimbali ni wa kutosha.

Bodi inaweza kukutana kwa ajili ya kufanya shughuli, kuahirisha na vinginevyo kudhibiti mikutano yake itakavyoona inafaa. Mikutano ya bodi inafanyika mara kwa mara kuitia mkakati, ufanisi wa kiuendeshaji na kifedha, na vilevile usimamizi. Mikutano maalum ya bodi inaweza kufanyika wakati itakapohitajika.

Kamati ya Uteuzi hufanya mapitio ya utaratibu wa mwendelezo wa majukumu ya bodi na kamati zake ili kuhakikisha kuwa zina watu sahihi wenye ujuzi na uzoefu kwa siku zijazo. Mkurugenzi Mtendaji ana wajibu wa kuhakikisha kuwa wajumbe wa kamati ya uongozi wana ujuzi, mamlaka na rasilimali za kutosha kutekeleza mkakati wa kampuni.

Uwajibikaji

Bodi ina wajibu wa kuhakikisha kampuni inakuwa na mafanikio. Kazi yake ni kuongoza na kutoa maamuzi ya busara katika kuielekeza kufanikisha ukuaji endelevu na kufanya kazi kwa maslahi ya wanahisa.

Kwa mujibu wa utendaji bora, Mwenyekiti na Mkurugenzi mtendaji wana majukumu tofauti. Mwenyekiti anawajibu wa kuongoza Bodi, wakati Mkurugenzi Mtendaji anawajibika kusimamia uendeshaji wa kampuni.

Mwongozo wa Bodi unaeleza wajibu wake, ambao ni pamoja na:

- Kufanya uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji na Mkurugenzi wa Fedha;
- Kusimamia kwa karibu mwelekeo wa kimkakati wa Vodacom Tanzania;
- Kupitisha miradi mikubwa, ununuzi au mauzo ya vitu;
- Kufanya uamuzi wa busara kuhusu masuala ya biashara ya kampuni, mbali na menejimenti;
- Kuhakkisha kuwa miundo, sera na taratibu stahiki zinakuwepo;
- Kuhakkisha udhibiti wa ndani wa kampuni unakuwa na mafanikio;
- Kupitia na kutathmini dharura za kampuni;
- Kupitisha bajeti ya mwaka na mpango wa utekelezaji;
- Kupitisha matokeo ya pamoja ya fedha ya mwaka na ya muda na vilevile mawasiliano kwenda kwa wadau;
- Kupitisha muundo wa uongozi na mpango wa mwendelezo wa uwepo wa viongozi; na
- Usimamizi wa teknolojia ya habari.

Wakurugenzi

Katiba ya kampuni inaeleza kuwa wakurugenzi wanapaswa kustaafu kwa zamu na wanaweza kuchaguliwa tena baada ya kila miaka mitatu.

Mwenyekiti

Katiba inaitaka Bodi kumchagua Mwenyekiti kila mwaka. Bodi inaridhika kuwa Mwenyekiti anaweza kutimiza majukumu yake ipasavyo. Jaji (mstaafu) Thomas B. Mihayo aliteuliwa kuwa Mwenyekiti kuanzia tarehe 1 Novemba 2020. Uteuzi wa kushika nafasi hiyo ya uenyekiti utajadiliwa na Bodi baada ya muda wake wa sasa kuisha.

Kupata ushauri huru

Bodi inatambua kuwa inawezekana kukawa na wakati ambapo wakurugenzi wakaona kuwa ni muhimu kupata ushauri huru wa kitaalamu. Kampuni itagharamia huduma hii kwa mujibu wa utaratibu uliopo.



Shughuli za uongozi wa kampuni

Vodacom Tanzania PLC

Mikutano ya Bodi

Jedwali hapo chini linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi katika mikutano ya Bodi kwa mwaka huu.

Jina la Mkurugenzi	6 Mei 2021 Maalum	15 Julai 2021 Maalum	2 Novemba 2021 Maalum	20 Januari 2022 Maalum	15 Machi 2022
Jaji (mstaafu) Thomas B					
Mihayo (Mwenyekiti)	✓	✓	✓	✓	✓
Bi Margaret Ikongo	x	✓	✓	✓	✓
Bi Thembeka Semane	✓	✓	✓	✓	✓
Bi Winifred Ouko	✓	✓	✓	✓	✓
Bw Dejan Kastelic	✓	✓	✓	✓	✓
Bw Diego Gutierrez	✓	✓	✓	✓	✓
Bw Hisham Hendi	✓	✓	✓	R	R
Bw Jacques Marais	✓	✓	✓	✓	R
Bw Kenneth Gomado	✓	✓	✓	✓	R
Bw Matimba Mbungela	✓	✓	✓	✓	✓
Bw Nkateko Nyoka	✓	✓	✓	✓	✓
Bi Raisibe Morathi	✓	✓	✓	✓	✓
Bw Sitholizwe Mdlalose	—	—	—	✓	✓
Bi Hilda Bujiku	—	—	—	—	✓
Bw Sudhersan Ramasamy	—	—	—	—	✓

Angalizo:

- Hisham Hendi alijuzulu tarehe 1 Novemba 2021.
- Jacques Marais alijuzulu tarehe 1 Januari 2022.
- Kenneth Gomado alijuzulu tarehe 21 Januari 2022.
- Sitholizwe Mdlalose aliteuliwa tarehe 1 Novemba 2021.
- Hilda Bujiku aliteuliwa tarehe 1 Januari 2022.
- Sudhersan Ramasamy aliteuliwa tarehe 21 Januari 2022.

Mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji

Jedwali hapo chini linaonesha mahudhurio ya wajumbe katika mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji kwa mwaka huo.

Jina La Mjumbe	30 Aprili 2021 Maalum	15 Julai 2021 Maalum	2 Novemba 2021 Maalum	20 Januari 2022 Maalum	15 Machi 2022
Bi. Margaret Ikongo (Mwenyekiti)	x	✓	✓	✓	✓
Bi. Thembeka Semane	✓	✓	✓	x	✓
Bi. Winifred Ouko	✓	✓	✓	✓	✓

Mikutano ya Kamati ya Ujira

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wajumbe katika mikutano ya Kamati ya Ujira mwaka huu.

Jina La Mjumbe	31 Mei 2021	19 Agosti 2021	10 Novemba 2021	14 Machi 2022
Bi. Winifred Ouko (Mwenyekiti)		✓	✓	✓
Bw. Diego Gutierrez		✓	✓	x
Bw. Matimba Mbungela		✓	✓	✓

Mikutano ya Kamati ya Uteuzi

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wajumbe kwenye mikutano ya Kamati ya Uteuzi mwaka huu.

Jina la Mjumbe	18 Agosti 2021	14 Machi 2022
Jaji (mstaafu) Thomas B Mihayo (Mwenyekiti)	✓	✓
Bi. Margaret Ikongo	✓	✓
Bw. Winifred Ouko	✓	✓
Bw. Matimba Mbungela	✓	✓

M-Pesa Limited

Bw. Matimba Mbungela

Mikutano ya Bodii ya M-Pesa Limited

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi kwenye mikutano ya Bodii ya M-Pesa Limited mwaka huu.

Jina la Mkurugenzi	28 Mei 2021	18 Agosti 2021	10 Novemba 2021	14 Machi 2022
Bw. Sitoyo Lopokoiyt (Mwenyekiti)	x	✓	✓	✓
Bw. Christopher Williamson	✓	✓	✓	✓
Bw. Jacques Marais	✓	✓	✓	R
Bw. Olaf Mumburi	✓	✓	✓	✓
Bw. Epimack Mbeteni	✓	✓	✓	✓

Angalizo:

Jacques Marais alistaafu tarehe 1 Januari 2022.

Mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wajumbe kwenye mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji ya M-Pesa Limited mwaka huu.

Jina la Mjumbe	28 Mei 2021	18 Agosti 2021	10 Novemba 2021	14 Machi 2022
Bw. Christopher Williamson (Mwenyekiti)	✓	✓	✓	✓
Bw. Jacques Marais	✓	✓	✓	R
Bw. Olaf Mumburi	✓	✓	✓	✓

Angalizo:

Jacques Marais alistaafu tarehe 1 Januari 2022.



Taarifa ya Masuala ya Ujira 2022



Barua kutoka kwa Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira

Margaret Ikongo

Wapendwa Wanahisa pamoja na wadau wetu

Ninayo furaha, kwa niaba ya Bodi kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Ujira ya Vodacom Tanzania kwa mwaka 2022. Taarifa hii inatoa muhtasari wa falsafa na sera yetu inayohusu wakurugenzi watendaji na wasio watendaji, na kwa kifupi inaeleza namna sera ilivyotekelezwa katika kipindi cha mwaka.

Kazi yetu kama wajumbe wa Kamati ya Ujira ni kusaidia na kuishauri Bodi kuhusu masuala yanayohusiana na ujira wa wakurugenzi watendaji. Tunawajibika kuhakikisha kuwa falsafa na sera ya ujira inaunga mkono azma ya kampuni ya kutoa ujira ulio sawa na stahiki ambao utavutia, kubakiza na kutoa motisha kwa watendaji wenyewe uwezo wa hali ya juu, wenyewe jukumu la kuongeza thamani ya wanahisa kwa kutekeleza malengo ya kimkakati ya Kampuni. Tunaendelea kutathmini sera zetu za ujira na kuhakikisha tunatekeleza kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana ('CMSA') pamoja na kukidhi matakwa ya wanahisa.

Ukiangalia shughuli zetu kwa mwaka uliopita, kuna masuala matatu ninapenda kuyasisitiza:

- Inafurahisha sana kuona hatua tuliyopiga katika kutekeleza azma yetu ya kuongeza uwakilishi wa wanawake katika safu ya uongozi wetu. Tunajivunia uteuzi wa Bi Hilda Bujiku kuwa Mkurugenzi wa Fedha, na hivyo kuongeza uwakilishi wa wanawake katika kamati ya uongozi kufika 38.5%. Maandalizi

ya viongozi wa idara wa siku za usoni, pia yanazingatia utekelezaji wa azma hii. Kati ya viongozi wajao wanaoandaliwa, 67.5% ni wanawake.

- Tumetunukiwa cheti cha Mwajiri Bora Tanzania, huu ukiwa ni mwaka wa tano mfululizo, ikithibitisha utendaji wetu bora, tukiwa ni sehemu kundi la makampuni katika dunia, yenye fikra za siku zijazo ambayo yanakusudia kuwaangalia wafanyakazi wake katika namna iliyo bora, ili kupata matokeo bora ya kampuni kiutendaji.
- Uimara wa mikakati ya kukuza vipaji unadhihirika kwa uwepo wa wafanyakazi wetu watananza wakifanya kazi maeneo mengine ambapo wanne wapo Vodacom Afrika Kusini, na watano wapo Safaricom Ethiopia ambapo tunaendelea kusambaza uwanda wa huduma. Huu ni ushahidi dhahiri wa uwekezaji wetu katika ujuzi kwa wafanyakazi wetu.

Kamati imezingatia taratibu za utoaji wa taarifa kwa mujibu wa matakwa ya sheria ya Soko la Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994, na

imeridhika kuwa taarifa hii imekidhi miongozo ya uendeshaji wa kampuni za umma zilizoorodheshwa kwene soko la hisa nchini, sambamba na kuwa makini katika utoaji wa taarifa nyeti za kiushindani.

Ninapenda kutoa shukrani kwa wajumbe wenzangu wa kamati kwa kuendelea kuniunga mkono, na ninataraja kuendelea kufanya kazi nao mwaka ujao.

Margaret Ikongo
Mwenyekiti wa mpito wa Kamati ya Ujira
12 Julai 2022

Kulingana na miongozo ya Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana kuhusu taratibu za usimamizi wa makampuni ya umma yaliyoordheshwa nchini Tanzania, taarifa hii inaeleza sera za Vodacom Tanzania za ujira kwa wakurugenzi watendaji na wakurugenzi wasio watendaji hususan kiasi na aina za ujira kwa wakurugenzi ikiwa ni pamoja na wakurugenzi wasio watendaji kwa pamoja.

Falsafa, sera na mfumo wetu wa ujira kwa mwaka huu kwa wakurugenzi watendaji.

Lengo letu ni kuwavutia, kuwawezesha kubaki na kuwapatia motisha watendaji wenye uwezo wa hali ya juu, sambamba na kulinganisha ujira wao na maslahi ya wanahisa na taratibu bora za utekelezaji.

Utaratibu wetu wa stahiki za ajira ni mpana, wenye ulinganifu kwenye vipengele vifuatavyo:

- Ujira wa uhakika (GP);
- Motisha ya muda mfupi (STIP);
- Motisha ya muda mrefu (LTIP);
- Programu mbalimbali za utambuzi;
- Fursa mbalimbali za kujifunza na kuijendeleza;
- Mazingira ya kazi yanayovutia; na
- Programu nzuri ya ustawi wa wafanyakazi.

Viongozi watendji wanafuata falsafa ya 'Jumla ya gherama kwa kampuni', ambayo tunairejelea kama ujira uhakika (GP). Michango katika huduma za tiba, fedha za ustaafu na mafao ya bima yamejumuishwa katika GP.

Vipengele hivyo hapo juu vinaendana na kuimarishwa kwa utaratibu wetu wa kutathmini utendaji kazi na kuendeleza vipaji. Sera yetu ni kuwapa marupurupu viongozi wetu watendaji kutokana na michango yao katika ufanisi wetu kimkakati, kifedha na kiutendaji. Ili kuwa muajiri anayeheshimika katika sekta yetu tunahitaji kuvutia, kuendeleza na kubakiza vipaji bora na rasilimali ya wataalamu wa ndani na kimataifa.

Kila mwaka tunalinganisha viwango na kuongeza malipo katika GP kulingana na soko, ufanisi binafsi na uwezo. Tathmini ya ufanisi binafsi na uwezo wa kiutendaji hubainishwa

kupitia utaratibu wetu wa kupima utendaji na uwezo wa kiutendaji wa wafanyakazi wetu. Matokeo ya utaratibu huu, huchangia katika uamuzi wa mabadiliko ya motisha ya muda mfupi na muda mrefu.

Motisha yetu ya muda mfupi inayolipwa kama bonasi ya fedha taslimu hutokana na kufikia malengo kwenye utendaji wa masuala ya fedha, mikakati, uendeshaji wa vitengo na malengo binafsi ambayo kila mtendaji amepewa. Kiasi kilichopo kwa ajili ya motisha ya muda mfupi kinatokana na utendaji kwenye masuala ya fedha kadiri ya malengo yaliyowekwa na kukubaliwa.

Viongozi watendaji ambao wametumwa kufanya kazi Vodacom Tanzania kutoka Vodacom Group Limited, hulipwa motisha ya muda mrefu kwa mujibu wa taratibu za kundi la makampuni la Vodacom Group, ambapo hupewa umiliki wa hisa na mwajiri wao. Hii huchochaea utendaji unoakisi umiliki na uaminifu, na huchangia katika lengo la Vodacom la kuwabakiza watendaji hodari. Mfumo huo ni mfumo kamili wa umiliki, na matokeo yake wahusika hupata gawio kutoka siku walipopewa hisa japokuwa thamani ya hisa inaweza tu kupatikana baada ya miaka mitatu na ni kwa kulingana na kiwango ambacho masharti ya kupewa hisa hizo yametimizwa.

Taarifa za ujira wa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji

Ujira wa wakurugenzi watendaji – Malipo ya Uhakika

Ujira wa wakurugenzi watendaji ulifanyiwa mapitio kwa kuzingatia ulinganishi na ujira wa watendaji wengine katika soko, na pia athari za kushindwa kuwabakiza watendaji muhimu katika menejimenti.

Kwa kuzingatia utaratibu/sera ya ujira, taarifa iliyo kwenye toleo hili ni kwa wakurugenzi waliostahili, ambapo maamuzi yote yanayohusu ujira yamefanywa kwa kuzingatia utaratibu wa ujira kama uliyopitishwa wakati uliopita na wanahisa. Kama ilivy kwa mwaka ultiangulia, hakuna mabadiliko yaliyofanywa katika utekelezaji wa sera/ utaratibu wa ujira katika mwaka huu.

Taarifa za ujira wa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji zimetolewa kwa muhtasari katika jedwali hapo chini na pia zimewasilishwa katika Maeleo 34 katika taarifa za pamoja za fedha na taarifa binafsi za fedha za kampuni (nakala ya kiingereza) yaliyopo katika ukurasa wa 132.

Bodi	Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji	Ujira	Uteuzi	Jumla
Wakurugenzi				
TB Mihayo	150 000			150 000
M Ikongo	30 000	15 000		45 000
W Ouko	30 000	8 000	12 000	53 000
T Semane	30 000	8 000		38 000
D Gutierrez ¹	30 000		4 000	34 000
M Mbungela ¹	30 000		4 000	37 000
N Nyoka ¹	30 000			30 000
D Kastelic ¹	30 000			30 000
S Ramasamy ¹	30 000			30 000
R Morathi ¹	30 000			30 000
S Mdlalose				0
H Bujiku				0
				477 000

1. Ada za ukurugenzi zinalipwa kwenda 'Vodacom group' na si kwa mkurugenzi binafsi.

Kiasi hiki ni jumla ya ada kwa dola ya Marekani, ikijumuisha kodi zote pamoja na kodi ya zuio, inayolipwa kwa shilingi ya Kitananzia kwa wakurugenzi wazawa, randi ya Afrika Kusini kwa wakurugenzi wakazi wa Afrika Kusini na dola ya Marekani kwa wakurugenzi wengine. Ada hii inalipwa kila robo mwaka kwa mikutano ya kawaida isiyopungua minne kwa mwaka, mikutano maalum mitatu na Mkutano Mkuu wa Mwaka na wa dharura kama itahitajika.

Taarifa ya Mkutano Mkuu

Vodacom Tanzania Public Limited Company

(Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)

(Namba ya usajili 38501)

(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)

('Vodacom Tanzania' au 'Kampuni')

Taarifa inatolewa kuwa, mkutano mkuu wa sita wa Kampuni kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2022 utafanyika kwa njia ya kielektroniki siku ya Alhamisi tarehe 22 Septemba 2022 kuanzia saa nne asubuhi. Mkutano huu utajadili yafuatayo:

1. Kuthibitisha kumbukumbu

Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa tano uliofanyika tarehe 15 Oktoba 2021.

Azimio la kawaida namba 1

"ILIAMULIWA KUWA kumbukumbu za mkutano mkuu wa tano uliofanyika tarehe 15 Oktoba 2021 zimethibitishwa."

Nakala za kumbukumbu zinapatikana kwenye tovuti ya Kampuni www.vodacom.co.tz/investor-relations

2. Kupitisha taarifa za fedha za mwaka zilizokaguliwa

"Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa za fedha ikijumuisha kampuni zake tanzu, pamoja na ripoti ya wakaguzi huru na ya wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2022."

Azimio la kawaida namba 2

"ILIAMULIWA KUWA taarifa ya fedha zilizokaguliwa za Kampuni ikijumuisha kampuni zake tanzu, pamoja na ripoti ya wakaguzi huru na ya wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2022, zimepokelewa na kupitishwa."

Taarifa ya mwaka inapatikana katika tovuti ya Kampuni www.vodacom.co.tz/investor-relations

3. Uchaguzi wa wakurugenzi

Kwa kupitia maaazimio tofauti:

- 3.1 Bi Kanini Mutooni kuwa mkurugenzi huru kwa mujibu wa ibara ya 76 ya Katiba ya Kampuni. Wasifu wake upo katika ukurasa wa 37.
- 3.2 Bw. Sudhersan Ramasamy na Bw. Sitholizwe Mdlalose waliteuliwa kuwa wakurugenzi wasio watendaji kwa mujibu wa ibara ya 86 ya Katiba ya Kampuni kujaza nafasi zilizojitekeza katika Bodi na kuendelea kutekeleza majukumu ya kiofisi hadi mkutano wa kawaida unaofuata, na hivyo wanastahili kuchaguliwa tena. Wasifu wao upo katika ukurasa wa 36.
- 3.3 Bi Hilda Bujiku aliteuliwa kuwa mkurugenzi wa Kampuni kwa mujibu wa ibara ya 86 ya Katiba ya Kampuni kujaza nafasi iliyojitekeza katika Bodi na kuendelea kutekeleza majukumu ya kiofisi hadi mkutano wa kawaida unaofuata, na hivyo anastahili kuchaguliwa tena. Wasifu wake upo katika ukurasa wa 36.
- 3.4 Bi Margaret Ikongo na Bw Nkateko Nyoka wanastahili kustaa fu katika mkutano huu kwa mujibu wa ibara 104 na 105 za Katiba ya Kampuni. Ibara hizo zinabainsha kuwa licha ya kustaa fu, wanaweza kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa wakurugenzi. Wasifu wao uko katika ukurasa wa 36.

Azimio la kawaida namba 3

"ILIAMULIWA KUWA Bi Kanini Mutooni amechaguliwa kuwa mkurugenzi huru."

Azimio la kawaida namba 4

"ILIAMULIWA KUWA Bw Sudhersan Ramasamy amechaguliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

Azimio la kawaida namba 5

"ILIAMULIWA KUWA Bw Sitholizwe Mdlalose amechaguliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

Azimio la kawaida namba 6

"ILIAMULIWA KUWA Bi Hilda Bujiku amechaguliwa kuwa mkurugenzi wa Kampuni."

Azimio la kawaida namba 7

"ILIAMULIWA KUWA Bi Margaret Ikongo amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi huru."

Azimio la kawaida namba 8

"ILIAMULIWA KUWA Bw Nkateko Nyoka amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

4. Uteuzi wa Ernst & Young kuwa wakagazi huru wa Kampuni

Kuteua kampuni ya Ernst & Young Inc., kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Ukagazi, Dharura na Utekelezaji, kuwa wakagazi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mukutano mkuu ujao wa mwaka.

Azimio la kawaida namba 9

"ILIAMULIWA KUWA Ernst & Young Inc. imeteuliwa kuwa mkagazi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mukutano mkuu ujao wa mwaka."

5. Uteuzi wa wajumbe wa Kamati ya Ukagazi, Dharura na Utekelezaji

Kupitia maazimio tofauti na kwa mujibu wa kifungu cha 32(f) cha Katiba ya Kampuni, Bi Margaret Ikongo, Bi Thembeka Semane wakiwa wajumbe wa Kamati ya Ukagazi, Dharura na Utekelezaji wachaguliwe kuendelea kuwa wajumbe na kumchagua Bi Kanini Mutooni kuwa mjambe wa kamati tajwa. Wasifu wao uko katika ukurasa wa 36 na 37.

Azimio la kawaida namba 10

"ILIAMULIWA KUWA Bi. Margaret Ikongo amechaguliwa kuendelea kuwa mjambe wa Kamati ya Ukagazi, Dharura na Utekelezaji."

Azimio la kawaida namba 11

"ILIAMULIWA KUWA Bi. Thembeka Semane amechaguliwa kuendelea kuwa mjambe wa Kamati ya Ukagazi, Dharura na Utekelezaji."

Azimio la kawaida namba 12

"ILIAMULIWA KUWA Bi. Kanini Mutooni amechaguliwa kuwa mjambe wa Kamati ya Ukagazi, Dharura na Utekelezaji."

6. Gawio

"Kuthibitisha kuwa hakutakuwa na malipo ya gawio kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2022."

Azimio la kawaida namba 13

"ILRIDHIWA KUWA hakutakuwa na malipo ya gawio kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2022."

7. Ada ya wakurugenzi

Kuidhinisha ada ya wakurugenzi wasio watendaji ya dola za Kimarekani 477 000 hadi hitimisho la mukutano mkuu ujao wa mwaka, ili kuiwezesha Kampuni kuwavutia watu wenye uwezo, ujuzi na uzoefu unaotakiwa ili kutoa mchango unaofaa kwa Kampuni. Hakuna mapendekezo ya mabadiliko ya ada.

Azimio la kawaida namba 14

"ILIAMULIWA KUWA kiwango cha ada ya mwaka ya wakurugenzi wasio watendaji cha dola za Kimarekani 477 000 kimeidhinishwa kwa mchanganuo ufuata:

	Pendekezo la ada Dola ya Marekani ¹	Ada ya sasa Dola ya Marekani
Mwenyekiti wa Bodii	150 000	150 000
Mjumbe wa Bodii	30 000	30 000
Mwenyekiti wa Kamati ya Ukagazi, Dharura na Utekelezaji	15 000	15 000
Mjumbe wa Kamati ya Ukagazi, Dharura na Utekelezaji	8 000	8 000
Mwenyekiti wa Kamati ya Ujiraa	12 000	12 000
Mjumbe wa Kamati ya Ujiraa	4 000	4 000
Mjumbe wa Kamati ya Uteuzi	3 000	3 000

1. Ada hii inajumuisha kodi zote ikijumuisha kodi ya zuio, inayolipwa kwa shilingi ya Kitanzania kwa wakurugenzi wazawa, randi ya Afrika Kusini kwa wakurugenzi wa Afrika Kusini na dola ya Marekani kwa wakurugenzi wengine. Ada hii inalipwa kila robo mwaka (kwa mikupuo minne) kwa mikutano ya kawaida isiyopungua minne kwa mwaka, mikutano maalum mitatu na Mkutano Mkuu wa Mwaka na wa dharura kama itahitajika.

Taarifa ya Mkutano Mkuu inaendelea

Wasifu wa Wajumbe wa Bodi



Hilda Bujiku (43)

Mkurugenzi wa Fedha - Vodacom Tanzania PLC

Cheti cha Taaluma ya Uhasibu (CPA) kutoka Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania.

Shahada ya Biashara(Uhasibu) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Programu kwa Maafisa wa juu wa Vodacom - Taasisi ya Sayansi ya Biashara ya Gordon, Afrika Kusini.

Hilda ni Mkurugenzi wa Fedha wa Vodacom Tanzania PLC tangu Januari 2022. Alijunga na Vodacom Tanzania mwaka 2012 na kushika nyadhifa mbalimbali za juu katika kampuni ikijumuisha Naibu Mkurugenzi wa Fedha anayehusika na Mipango na Uchambuzi wa Fedha, Mahusiano ya Wawekezaji na Sekretarieti ya Kampuni. Baadaye alihamishiwa Lesotho kama Mkurugenzi wa Fedha. Hilda ana uzoefu wa zaidi ya miaka 16 akifanya kazi katika kampuni za mawasiliano ya simu.



Sitholizwe Mdälose (42)

Mkurugenzi asiyi mtendaji

Shahada ya Uhasibu (BCompt), Chuo Kikuu cha Afrika Kusini

Mwanachama wa Shirikisho la Wanataluma ya Uhasibu, Uingereza (ACCA).

Mhitimu wa Programu ya Uongozi, Shule ya Biashara Harvard.

Sitholizwe ni Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom South Africa (VSA) akitokea Vodacom Tanzania ambako alikuwa Mkurugenzi Mtendaji tangu Novemba 2021. Sitholizwe ameshika nafasi mbalimbali za juu za uongozi ndani ya Vodacom Group zikiwemo Kaimu Afisa Mkuu wa Fedha pamoja na Afisa Mkuu wa Fedha wa Vodacom International Business. Kabla ya hapo, Sitholizwe alikuwa Vodafone Group kwa zaidi ya miaka 6 akishikilia nafasi mbalimbali za uongozi wa juu. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 19 katika fani ya usimamizi na ushauri wa fedha; ambayo miaka 13 akiwa katika sekta ya mawasiliano ya simu ya masoko yaliyokua pamoja na yale yanayoibukia. Aliteuliwa kuwa mkurugenzi wa Bodii ya Vodacom Tanzania mwezi Julai 2022.



Sudhersan Ramasamy (36)

Mkurugenzi asiyi mtendaji

Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara kutoka Taasisi ya Teknolojia (IIT) Kharagpur, India

Shahada ya Uhndisi Mitambo kutoka Chuo cha Anna India, na

Cheti cha taaluma ya uchambuzi wa masuala ya fedha kutoka CFA Institute, Marekani;

Bw Ramasamy ni Afisa Mkuu wa Fedha – Vodacom International Business. Ameshika nafasi mbalimbali za juu za uongozi ndani ya Vodacom Group kwa zaidi ya miaka 12. Kabla ya uteuzi huu Bw Sudhersan alikuwa Mkuu wa Mipango ya Fedha na Uchambuzi ambapo alishughulika na mchakato wa utayarishaji bajeti na maoteo ya kampuni ya kampuni ya Vodacom South Africa, ikijumuisha mpango wa biashara wa muda mrefu na usimamizi wa utayarishaji wa mikakati. Kabla ya hapo alikuwa Meneja Mkazi wa makampuni yaliyo chini ya Vodafone kanda ya AMAP akishughulika na usimamizi wa menejimenti na utawala bora. Vilevile, alishika nafasi mbalimbali kama mshauri wa masuala ya fedha na biashara katika makampuni ya Vodafone India na Vodafone Quarat. Aliteuliwa kuwa mkurugenzi wa bodii ya Vodacom Tanzania mwezi Januari 2022.



Nkateko Nyoka (58)

Mkurugenzi asiyi mtendaji

Shahada ya Uzamili ya Sheria na Utawala wa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Harvard

Shahada ya Sheria pamoja na cheti cha uwakili (Baccalaureus Procurationis (B.Proc)) kutoka Chuo cha Witwatersrand, Johannesburg.

Bw Nyoka ni Afisa Mkuu wa Sheria, Kanuni na Dharura wa Vodacom Group Limited, Afrika Kusini. Kabla ya kuijunga na Vodacom Group, alishika nyadhifa mbalimbali za uongozi MTN (Pty) Limited na MTN Group Limited pamoja Taasisi ya Jamii ya MTN, Afrika Kusini. Pia Bw Nyoka alikuwa Afisa Mkuu Mtendaji wa kampuni ya Independent Communications Authority of South Africa (ICASA) ambapo alitoa mchango mkuropa uliowezesha mazingira ya ushindani katika sekta ya mawasiliano ya Afrika ya Kusini. Bw Nyoka pia ni mkurugenzi wa bodii ya Vodacom Lesotho, Vodacom Msunduzi na Vodacom DRC. Aliteuliwa kuwa mkurugenzi wa bodii ya Vodacom Tanzania mwezi Aprili 2020.



Margaret Ikongo (65)

Mkurugenzi huru

Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara na masuala ya Fedha, Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Cheti cha Kimataifa cha Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Taasisi ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Uingereza.

Diploma ya Kimataifa ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi na Mjumbe Mhitimu wa Taasisi ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Uingereza. Mjumbe katika Taasisi ya masuala ya Bima, Uingereza.

Margaret aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Pia ni mjumbe wa bodii ya wakurugenzi ya Actuarial and Risk Consulting, na Metrolife and Meticulus Insurance. Kabla ya hapo, Margaret alikuwa kwenye Bodii za NMB Plc, AAR Insurance Tanzania pamoja na Bodii ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Bodii ya NMB Bank PLC. Margaret ana uzoefu mkubwa katika masuala ya fedha na utawala bora akiwa ameupata kutokana na kufanya kazi katika sekta ya bima ambapo alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Taifa kwa kupindi cha miaka kumi. Margaret pia alikuwa mshauri wa Karmishna wa Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania pamoja na Kaimu Mkuu wa Kurugenzi ya Ufundji.

Thembeka Semane (46)

Mkurugenzi huru

Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Chuo cha Monash Afrika Kusini; Stashahada ya Juu katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Biashara cha Pretoria Gordon, Afrika Kusini Mwanachama wa Taasisi ya Taaluma ya Benki ya Afrika Kusini.

Thembeka aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Thembeka ana uzoefu katika masuala ya biashara ukihusisha mikakati ya mashirika, utekelezaji wa mifumo ya biashara, miradi yenye thamani kubwa, utekelezaji na ufuataliaji, utawala bora na vilevile usimamizi wa fedha. Thembeka ni mkurugenzi wa Linea Consulting (Pty) Ltd, mjumbe wa Kamati ya Huduma ya ACASA & ATNS, akiripoti kwa Waziri wa Usafirishaji wa Afrika Kusini. Hivi sasa, ni mjumbe katika bodi ya Mamlaka ya Huduma ya Nishati ya Afrika Kusini (NERSA), mjumbe wa kamati ya ukaguzi wa kampuni zinazomilikiwa na serikali (North West Government) pamoja na kampuni ya MOGS (Pty). Pia ni mjumbe wa bodi na mjumbe wa Baraza la ICASA. Thembeka anaafanya kazi kama mjumbe wa bodi wa Idara ya Makazi EAAB, Mwenyekiti wa Kamati yake ya Fedha na Uwekezaji na ni mjumbe wa Kamati za Ukaguzi na Dharura pamoja na ya Rasilimaliwatu na Ujira.

Kanini Mutooni (46)

Elimu ya utekelezaji wa Sera za Kimataifa, Shule ya masuala ya kiserikali ya Harvard
Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara na masuala ya Fedha, Chuo Kikuu cha City, London.
Diploma ya masuala ya Dhamana (Uingereza)
Cheti cha Taaluma ya Uhaisbu (ACCA) Uingereza
Shahada ya Biashara, Chuo Kikuu cha Kikatoliki, Kenya

Kanini alikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya The Global Innovation Fund, chombo cherye uwekezaji wa Dola za Marekani 250 Milioni kinachoungwa mkono na serikali za Uingereza, Marekani, Canada, Australia and Sweden. Hivi sasa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Draper Richards Kaplan Foundation akisimamia Afrika. Pia ni mjumbe katika Bodi za Financial Sector Deepening Africa (FSDA); MCE Social Capital, the United Nations Capital Development Fund, Africa Enterprise Challenge Fund, Amref Health Innovation na CDC UK PLC. Kabla ya hapo, Kanini alikuwa mjumbe wa Bodи katika benki za uwekezaji huko Uingereza na Marekani ikiwa ni pamoja na Bank of America-Merrill Lynch na Dresdner Kleinwort Benson.

Tarehe ya kufunga rejesto

Tarehe ya kufungwa rejesto ya wanahisa wa Kampuni kwa madhumuni ya kustahili kuhuduria, kushiriki na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni Alhamisi 15 Septemba 2022.

Kushiriki kwa njia ya kielektroniki

Mkutano mkuu wa nne wa wanahisa utafanyika kwa njia ya kielektroniki kama ilivyoainishwa kwenye kifungu 29 na 63 cha Katiba ya Kampuni.

Mkutano mkuu utaoneshwa mubashara kuitia kiunga cha wavuti kwenye simu janja. Wanahisa waliopo kwenye rejesto itakayofungwa tarehe 15 Septemba 2022 wataweza kujisajili ili kushiriki katika mkutano mkuu. Muongozo wa namna ya kushiriki kwa njia ya kielektroniki pamoja na kujisajili ili kuweza kupata neno la siri utawekwa kwenye tovitu ya Kampuni <https://vodacom.co.tz/investors>. Kwa taarifa zaidi tafadhalii wasiliana nasi kuitia 0800750164.

Wanahisa watawajibika kwa gharama za data na mtandao. Kampuni haitawajibika na upotevu wa mawasiliano kutokana na matatizo ya kintandao/kuishiwa muda wa hewani/kukatika kwa umeme/na matatizo ya kiufundi ya kielektroniki yanayoweza kuathiri ushiriki wa mwanahisa kwenye mkutano mkuu mwaka kwa njia ya mtandao.

Wanahisa wanahimizwa kutuma maswali yatokanayo na maazimio yaliyopo kwenye taarifa hii kabla ya mkutano mkuu kwenda kwenye barua pepe investorrelations@vodacom.co.tz kabla ya Jumatatu ya tarehe 19 Septemba 2022 saa 4:00 asubuhi. Majibu ya maswali hayo yatatolewa katika mkutano mkuu. Uwasilishaji wa maswali haumzuii mwanahisa kuuliza maswali siku ya mkutano mkuu.

Mahudhurio

Wanaostahili kuhuduria, kuzungumza na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni wanahisa tu.

Wanahisa wanaweza kuteua wawakilishi kuhuduria, kutoa maoni na kupiga kura kwa niaba yao. Mwakilishi si lazima awe mwanahisa wa Kampuni. Fomu ya uwakilishi iliyojazwa pamoja na nakala ya hati ya hisa au risiti ya uwekezaji ya DSE ya mwanahisa, kitambulisho cha taifa/kura/leseni ya udereva na taarifa za mawasiliano vitumwe kwa barua pepe kwenda investorrelations@vodacom.co.tz au viwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni katika ghorofa ya 7, Vodacom Tower, Ursino Estate, Kiwanja namba 23, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanzania kabla ya saa 4:00 asubuhi Jumatatu ya tarehe 19 Septemba 2022. Fomu ya uwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya Kampuni <https://vodacom.co.tz/investors>.

Upigaji kura utaendeshwa kulingana na Katiba na kanuni za Kampuni. Maazimio ya kawaida yatakayopitishwa katika mkutano mkuu huu yatapaswa kuungwa mkono na zaidi ya 50% ya kura za wanahisa. Azimio maalum litapaswa kuungwa mkono na angalau 75% ya kura za wanahisa.

Wanahisa wenyi hisa zisizo kwa majina yao lazima wawapatie watanzaji au wawakilishi wao maelekezo ya kupiga kura katika mkutano mkuu wa mwaka. Kama mtunzaji au mwakilishi wako hatapokea maelekezo kutoka kwako, kama itakavyokuwa, itabidi kufanya maamuzi kulingana na mamlaka uliyoyatoa kwake.

Uwasilishaji wa fomu ya mwakilishi haumzuii mwanahisa kuhuduria mkutano mkuu wa mwaka.

Imeidhinishwa na Bodи

Caroline M Mduma
Katibu wa Kampuni
31 Agosti 2022



Fomu ya Mwakilishi

Vodacom Tanzania PLC

(Imesajiliwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
 (Namba ya Usajili 38501)
 (ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)
 ("Vodacom" au "Kampuni")

Kifungu A Ijazwe na wanahisa wote

Jina Kamili

Namba ya hati ya hisa (CDS A/c No)

Idadi ya hisa mwanahisa anazomiliki

Kifungu B Ijazwe na wanahisa watakaoteuwa wawakilishi (na si Mwenyekiti) kuhudhuria mkutano kwa niaba yao

Mimi(Sisi), mwenye/wenye hati ya hisa zenyet idadi ya hisa za kampuni kwa mujibu wa kifungu A, namteua/tunamteua (angalia maelekezo namba 1&2)

au akishindwa ye ye

au akishindwa ye ye

Mwenyekiti wa mkutano mkuu wa mwaka kuwa mwakilishi wangu/wetu kuhudhuria, kushiriki mijadala na kupiga kura kwa niaba yangu/yetu katika mkutano mkuu wa mwaka wa sita utakaofanyaika kwa nji ya kielektroniki siku ya Alhamisi, tarehe 22 Septemba 2022 kwa lengo la kutoa maamuzi na kuitisha maazimio ya kawaida, kupiga kura ya kuafiki au kutokuaufiki au kutoshiriki kwenye upigaji kura kulingana na hisa zilizoandikishwa kwa jina langu/letu.

Kifungu C Ijazwe na wanahisa wote

Weka alama x kwenye kisanduku kulingana na matakwa yako.

Vinginevyo mwakilishi wako atapiga kura atakavyona inafaa.

	Naafiki	Siafiki	Sishiriki
1. Azimio ka kawaida namba 1			
Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa mwaka uliofanyaika tarehe 15 Oktoba 2021			
2. Azimio la kawaida namba 2			
Kupitisha taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2022			
3. Azimio la kawaida namba 3			
Kumchagua Kanini Mutooni kuwa mkurugenzi huru			
4. Azimio la kawaida namba 4			
Kumchagua Sudhersan Ramasamy kuwa mkurugenzi asiye mtendaji			
5. Azimio la kawaida namba 5			
Kumchagua Sitholizwe Mdlalose kuwa mkurugenzi asiye mtendaji			
6. Azimio la kawaida namba 6			
Kumchagua Hilda Bujiku kuwa mkurugenzi wa Kampuni			
7. Azimio la kawaida namba 7			
Kumchagua tena Margaret Ikongo kuwa mkurugenzi huru			
8. Azimio la kawaida namba 8			
Kumchagua tena Nkateko Nyoka kuwa mkurugenzi asiye mtendaji			
9. Azimio la kawaida namba 9			
Kuchagua Ernst & Young Inc. kuwa wakaguzi wa Kampuni kwa mwaka unaoishia Machi 2023			
10. Azimio la kawaida namba 10			
Kumchagua tena Margaret Ikongo kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji			
11. Azimio la kawaida namba 11			
Kumchagua tena Thembeka Semane kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji			
12. Azimio la kawaida namba 12			
Kumchagua Kanini Mutooni kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji			
13. Azimio la kawaida namba 13			
Kuthibitisha kuwa hakutakuwa na malipo ya gawio kwa mwaka ulioishia terehe 31 Machi 2022			
14. Azimio la kawaida namba 14			
Kuidhinisha ada ya mwaka ya wakurugenzi wasio watendaji ya dola za Kimarekani 477 000 kwa mwaka			

Imetiwa sahihi tarehe

mwezi Septemba 2022

Sahihi:

Sahihi:

Fomu ya mwakilishi iliyojazwa iwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni ya Vodacom Tanzania PLC kabla saa 4 asubuhi, Jumatatu tarehe 19 Septemba 2022.

Maelekezo ya fomu ya mwakilishi

1. Mwanahisa anayepaswa kuhuduria katika mukano mkuu anaweza kuteua mwakilishi wake kuhuduria, kutoa maoni na kupiga kura kwa niaba yake. Mwakilishi sio lazima awe mwanahisa wa kampuni. Kwa makampuni, fomu ya mwakilishi ijazwe na afisa mwenye mamlaka na iwekwe muhuri wa Kampuni husika.
2. Weka alama 'X' kwenye eneo la kujaza kwenye fomu kulingana na kura unayotaka kupiga katika agenda husika. Iwapo utapenda kupiga kura kwa hisa pungufu ya hisa unazomiliki, onyesha idadi ya hisa pungufu ambazo ungependa zipige kura. Iwapo maelekezo haya hayatazingatiwa, mwakilishi atapiga kura atakavyoona inafaa.
3. Mwanahisa anaweza kuweka jina la mwakilishi/wawakilishi wake kwenye sehemu iliyoonyeshwa kwenye hii fomu bila kufuta kipengele cha kuwakilishwa na "Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa mwaka" kilichopo chini ya sehemu ya kuandika majina ya wawakilishi. Mwanahisa atapaswa kuweka sahihi yake iwapo atafuta kipengele hicho. Mwakilishi ambaye jina lake limejazwa likiwa la kwanza kwenye fomu ya uwakilishi akihuduria mukano mkuu ndiye atahusika kufanya maamuzi.
4. Fomu za mwakilishi zilizojazwa pamoja na hati ya hisa au risiti ya uwekezaji ya DSE ya mwanahisa, ziwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni - ghorofa ya 7, Vodacom Tower, Ursino Estate, Kiwanja na 23, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanzania kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Jumatatu tarehe 19 Septemba 2022. Aidha, fomu zinaweza kusainiwa kisha kuzituma kwa barua pepe ya investorrelations@vodafone.co.tz.
5. Mwanahisa akifanya masahihisho/mabadiliko yoyote kwenye fomu ya mwakilishi, atapaswa kuwekwa sahihi yake pemberi ya masahihisho/ mabadiliko haya.
6. Wenyе hisa wenye umri mdogo kisheria wanapaswa kusimamiwa na wazazi/walezi wao ambaо watapaswa kuwa na nyaraka za kisheria za kuwathibitisha.
7. Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa mwaka atakubali fomu ya mwakilishi itakavyokuwa imejazwa tofauti na matakwa haya iwapo ataridhika na namna ambavyo mwanahisa atapenda kupiga kura.
8. Kwa wale wenye hisa za pamoja/vikundi:
 - Yeyote kati yao anaweza kutia sahihi kwenye fomu hii
 - Kura ya mwanahisa mkubwa (ukubwa wa hisa utajulikana kulingana na majina yaliorodheshwa kwenye rejista ya wanahisa wa Kampuni) itakayopigwa na yeze binafsi au kutumia mwakilishi, ndio itakayoruhusiwa kwa niaba ya wanahisa wenzake kwenye kikundi.

Ms Caroline Mduma

Katibu wa Kampuni
Ghorofa ya 7, Vodacom Tower, Ursino Estate
Kiwanja na 23, Barabara ya Bagamoyo
P.O. Box 2369
Dar es Salaam
Barua pepe: investorrelations@vodafone.co.tz

Taarifa kuhusu umiliki

Jumla ya hisa	# ya hisa	% ya hisa
Vodacom Group Limited	1 680 000 200	75.0%
Mfuko wa Pensheni wa Wafanyakazi wa Serikali (Uwekezaji wa Shirika la Umma SOC Limited, Jamhuri ya Afrika Kusini)	164 503 540	7.3%
Wawekezaji wa Kitaasisi (Afrika Mashariki)	250 357 692	11.2%
Wawekezaji wa Kitaasisi (Sehemu nyingine duniani)	50 062 653	2.2%
Wawekezaji wengine ¹	95 076 215	4.3%
	2 240 000 300	100.0%

1. Hisa hizi zinaweza kuhusisha uwekezaji kutoka kwenyw taasisi au watu binafsi ambazo ziko chini ya kiwango cha uainishaji (Uchanganuzi).

Umiliki wa hisa kitaasisi	% Umiliki kitaasisi
Tanzania	47.9%
PIC	35.4%
Uganda	6.0%
Wanahisa wengine wa kimataifa	10.7%
	100.0%

Taarifa za Kampuni

Vodacom Tanzania Public Limited Company

(Imeandikishwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
Usajili namba: 38501
(ISIN: TZ1996102715 Share Code: VODA)

Directors

TB Mihayo (Mwenyekiti)¹
S Mdlalose (Mkurugenzi Mtendaji)²
H Bujiku (Mkurugenzi wa Fedha)¹
D Kastelic³
D Gutierrez⁴
M Ikongo¹
M Mbungela⁵
N Nyoka⁵
R Morathi⁵
S Ramasamy⁶
T Semane⁵
W Ouko⁷
1. Mtanzania 2. Muingereza 3. Mslovenia 4. Mbolivia
5. Mwfrika Kusini 6. Mhindi 7. Mkenya

Katibu wa Kampuni

Caroline Mduma
Ghorofa ya 15, Vodacom Tower,
Eneo la Ursino, Kiwanja namba 23, Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2369, Dar es Salaam, Tanzania

Ofisi iliyosajiliwa

Ghorofa ya 15, Vodacom Tower,
Eneo la Ursino, Kiwanja namba 23, Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2369, Dar es Salaam, Tanzania

Mkaguzi wa Hesabu za Fedha

Ernst & Young
Ghorofa ya 4, Tanhouse Tower
Kiwanja namba 34/1, Ursino Kusini
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2475
Dar es Salaam, Tanzania

Watoa huduma za Kibenki

Citibank Tanzania Limited

Citibank House
Kiwanja namba 1962, Barabara ya Toure, Oysterbay
S.L.P 71625
Dar es Salaam, Tanzania

National Bank of Commerce Limited

Barabara ya Sokoine & Mtaa wa Azikiwe
S.L.P 1863
Dar es Salaam, Tanzania

NMB Bank Plc

Mtaa wa Ohio /Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 9213
Dar es Salaam, Tanzania

CRDB Bank Plc.

Mtaa wa Azikiwe
S.L.P 268
Dar es Salaam, Tanzania

Standard Chartered Bank Tanzania

Jengo la International House
Mtaa wa Shaaban Robert/Garden Avenue
S.L.P 9011
Dar es Salaam, Tanzania

Washauri wa Mambo ya Kisheria

IMMMA (Advocates)

Kiwanja namba 357, IMMMA House
Barabara ya Umoja wa Mataifa, Upanga
S.L.P 72484
Dar es salaam, Tanzania

Lawhill

14112 Regent Estate Mikocheni
Mtaa wa Historia, Kiwanja namba 311,
Nyumba namba 96
S.L.P 105646
Dar es salaam, Tanzania

Msajili Masuala ya Hisa

CSD & Registry Company Limited
Soko la Hisa la Dar es Salaam
Ghorofa ya 3, Kambarage House
Mtaa wa 6 Ufukoni
S.L.P 70081
Dar es Salaam, Tanzania

Mshauri Mkuu aliyesajiliwa

Orbit Securities Company Limited

Mawasiliano ya nje

Rosalynn Mworia

Mahusiano na Wawekezaji

Albert Maneno, Neema Munuo
investorrelations@vodafone.co.tz
www.vodafone.co.tz/investors

Dai la haki

Taarifa zisizofuata Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha ('IFRS')

Taarifa hii ina baadhi ya hatua zisizofuata Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha ambazo hazijapitiwa au kuripotiwa na wakaguzi wa Kundi la Kampuni za Vodacom ('Kundi'). Menejimenti ya Kundi inaamini hatua hizi zinatoa taarifa muhimu za ziada kwa kuelewa ufanisi wa Kundi la Vodacom au biashara za Kundi la Vodacom kwa sababu zinaeleza hatua zilizotumiwa na Kundi la Vodacom kutathimini ufanisi. Hata hivyo, taarifa hizi za ziada zilizowasilishwa hazikufasiliwa kwa njia inayofanana na kampuni zote, ikiwa ni pamoja na zile zilizo katika tasnia ya Kundi la Vodacom. Hivyo, inawezekana haiwezi kulinganishwa na hatua zinazofanana na kutolewa taarifa na kampuni nyingine. Kwa kuongezea, ingawa hatua hizi ni muhimu katika usimamizi wa biashara, hazipasvi kuangaliwa kipwekepweke au kama mbadala, badala yake ziwe kama kijalizo, katika hatua za Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha. Rejea katika sehemu ya 'Ufanisi wetu' ya taarifa hii kwa maelezo yanayohusiana na mapato ya huduma, EBIT na mapato kwa kila hisa.

Alama za Biashara

Vodafone, logo ya Vodafone, M-Pesa, Vodacom, Wakulima Waliounganishwa na Vodafone Supernet ni alama za biashara za Vodafone Group Plc (au ina program zinazosubiria). M-Fundi, M-Shamba, M-Pawa na Vodacom Faraja ni alama za biashara za Vodacom Tanzania Public Limited Company (au ina program zinazosubiria). Bidhaa zingine na majina ya kampuni yalijotajwa hapa yanaweza kuwa alama za biashara za wamiliki wao husika.

Matamko ya Matarajio

Taarifa hii, ambayo inajumuisha matokeo ya Kundi la makampuni kwa mwaka unoishia tarehe 31 Machi 2022, ina 'matamko ya matumaini', ambayo hayajapitiwa au kuripotiwa na wakaguzi wa Kundi, kuhusiana na hali ya kifedha ya Kundi, matokeo ya uendeshaji na biashara na taarifa zinazohusiana na mipango na malengo ya Kundi la Vodacom. Hasa, matamko haya ya kuangalia mbele yanajumuisha matamko yanayohusiana na: ufanisi wa baadaye wa Kundi la Vodacom; matumizi ya mtaji siku zijazo, ununuzi, kujitoa, gharama, mapato, masharti ya kifedha, sera ya gawio na maendeleo ya baadaye; mikakati ya biashara na uwekezaji inayohusiana na upanuzi na ukuaji wa Kundi la Vodacom; athari za udhibiti wa biashara za Kundi la Vodacom unaofanya na serikali katika nchi inapofanya shughuli zake; matarajio ya Kundi la Vodacom kuhusiana na tarehe za uzinduzi na kuanza uuzaji wa bidhaa, huduma au teknolojia; matarajio kuhusu mazingira ya uendeshaji na hali ya soko; ongezeko la wateja na matumizi; na kiwango cha ongezeko la gawio kwa Kundi.

Matamko ya kuangalia mbele wakati mwengine, lakini si wakati wote, hubainishwa kwa matumizi yao ya tarehe katika wakati ujao au Maneno kama 'nita', 'tarajia', 'kusudia', 'ninge', 'weza', 'paswa', 'amini', 'panga' au 'lenga' (pamoja na miundo yao ya ukarushii).

Kwa hali yao, matamko ya kuangalia mbele kwa asili yanatabirika, yanaweza kukiwa na yanajumuisha hatari na mashaka kwa sababu yanahusiana na matumio na yanategemea mazingira ambayo yanaweza kutokea au yasitokee siku za baadaye. Kuna sababu mbalimbali ambazo zinaweza kusababisha matokeo halisi na maendeleo kutofautiana kabisa kuanzia yale yaliyoelezwa au kumaanishwa na matamko haya ya kuangalia mbele. Sababu hizi ni pamoja na, ingawa haziishii hapo, zifuatazo: mabadiliko katika hali ya kiuchumi au kisiasa katika masoko yanayohudumiwa kwa shughuli za Kundi la Vodacom; ushindani mkubwa kuliko iliyotarajiwa; gharama kubwa kuliko iliyotarajiwa na kupungua kwa wateja wa kudumu; mabadiliko katika hali ya matumizi ya wateja wapya na waliopo; uwezo wa Kundi kupuanua nafasi yake kimawanda au kuongeza muda au kuchukua leseni mpya; uwezo wa Kundi kufanikisha kuokoa gharama; uwezo wa Kundi kutekeleza mkakati wake wa kutumia mkongo; kuanza kutoa bidhaa na huduma mpya; huduma za data (mobile data), upanuzi wa Biashara na mtandao wa 4G, mabadiliko katika viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, na vilevile katika viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, na vilevile viwango vya riba; uwezo wa Kundi kupata faida kutoekana na kuingia katika ubia au kufanya biashara pamoja na kuingia katika kufanya biashara ya huduma na utoaji wa leseni ya chapa; matokeo yasiyofaa kwa Kundi ya kufanya na kuchanganya ununuzi na utupaji; mabadiliko katika mfumo wa kisheria ambapo Kundi huendesha shughuli zake; athari za mashauri ya kisheria na mengineyo; kupoteza wasambazaji au kuvurugika kwa mnyororo wa usambazaji; maendeleo katika hali ya fedha ya Kundi, mapato na fedha zinazosambazwa na mambo mengine ambayo Bodi imezingatia wakati wa kuamua viwango vya magawio; uwezo wa Kundi kuwa na mtaji wa kufanya kazi na mahitaji mengine; mabadiliko katika viwango vya kodi kisheria au mchanganyiko wa faida; na/au mabadiliko katika sharia ya kodi. Matamko mengine yote yaliyofuata ya kuangalia mbele yawe kwa maandishi au mdomo ambayo ni ya Kampuni, kwa mhusika ye yote wa Kundi au kwa watu wowote wanaofanya kwa niaba yao wanastahili katika wingi wao kwa sababu zinarejelewa hapo juu. Uhakika hauwezi kutolewa kuwa matamko ya kuangalia mbele katika waraka huu yatafikiwa. Kutegemea kufuata sharia na kanuni zinazotumika, Kampuni haikusudii kuboresha matamko haya ya kuangalia mbele na haichukui wajibu wowote wa kufanya hivyo.

